ISSN 0856 – 034X

Supplement No. 21 *7th June, 2013*

SUBSIDIARY LEGISLATION

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 23 Vol. 94 dated 7th June, 2013

Printed by the Government Printer Dar es Salaam, by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 160 la tarehe 07/06/2013

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7(1) na 16(1))

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI, 2013

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada Ushuru) za Halmashauri ya Mji wa Bariadi za mwaka 2013 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye *Gazeti* la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:-

"ada na ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"bajaji" maana yake ni gari la abiria lenye matairi matatu;

"bidhaa" maana yake ni kitu chochote chenye thamani kilicholetwa sokoni au gulioni kwa lengo la kuuzwa.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Bariadi;

'kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

"kibali cha ujenzi" maana yake ni kibali cha ujenzi kinachotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia Kanuni za Ujenzi Mjini;

"leseni ya biashara" maana yake ni kibali cha maandishi kinachotolewa kwa mtu binafsi, kampuni au taasisi kinachoruhusu kufanya biashara au shughuli yoyote katika eneo la Halmashauri;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengewa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

Tangazo la Serikali Na. 160 (linaendelea)

"madini ya ujenzi" maana yake ni kokoto, mchanga na mawe;

"matangazo ya biashara" maana yake ni ishara, alama, maneno. yaliyobandikwa kwenye mabango, kuta za nyumba au vibao kwa lengo la kuitambua biashara fulani;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"masoko" maana yake ni sehemu maalumu iliyotengwa na kumilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya kuuza na kununua bidhaa au huduma kufuatana na taratibu zilizowekwa na Halmashauri;

"vibao vya Matangazo ya Biashara" maana yake ni vibao vilivyowekwa na wafanyabiashara kwa lengo la kutangaza biashara zao na ni pamoja na matangazo yaliyoandikwa au kubandikwa katika kuta za nyumba na magari;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

Ada na ushuru

4.—(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoorodheshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na ushuru unaotozwa chini ya sheria ndogo hizi unapaswa kulipwa kabla ya mlipaji kupata huduma husika.

(3) Tarehe ya mwisho ya kulipa ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi ni tarehe 25 hadi 30 ya kila mwezi.

Uteuzi wa Wakala

5.—(1) Halamshauri inaweza kumteua mtu binafsi, kampuni, asasi au taasisi kuwa wakala wa kukusanya ada na ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya sheria ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:-

(a) kukusanya na kupokea ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi:-

(b) kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri;

(c) kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya sheria ndogio hizi.

Wajibu wa mfanyabiashara

6. Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara:-

(a) kuweka eneo analofanyia biashara katika hali ya usafi muda wote;

(b) kulipa ushuru kama inavyotakiwa katika Sheria Ndogo hizi.

Makosa na adhabu

7. Mtu yeyopte atakayekwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungu kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili yaani na faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

8. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu yeyote isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kutenda kosa hilo kwa kujaza fomu maalum iliyopo kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini anayodaiwa.

SEHEMU A

ADA YA HUDUMA YA MACHINJIO

S/No.	*Mnyama*	*Kiasi*	*Idadi*
1.	Ng'ombe	Tsh. 1500/=	1
2.	Mbuzi / Kondoo	Tsh. 500/=	1
3.	Nguruwe	Tsh. 1000/=	1

SEHEMU B

ADA YA UKAGUZI WA NYAMA

S/No.	*Mnyama*	*Kiasi*	*Idadi*
1.	Ng'ombe	Tsh. 1500/=	1
2.	Mbuzi / Kondoo	Tsh. 800/=	1
3.	Nguruwe	Tsh. 800/=	1

SEHEMU C

USHURU NA USAJILI WA NGOZI

S/No.		*Ushuru*	*Idadi*
1.	I) Ushuru wa ngozi	Ng'ombe Tsh. 100/=	Kwa kila ngozi
		Mbuzi/Kondoo Tsh. 50/=	Kwa kila ngozi
2.	II) Usajili wa eneo la ngozi		
	Wakubwa	Tsh. 80,000/=	Kwa mwaka
	Wakati	Tsh. 40,000/=	Kwa mwaka
	Wadogo	Tsh. 20,000/=	Kwa mwaka

Tangazo la Serikali Na. 160 (linaendelea)

SEHEMU D

USHURU WA KUPIMA AFYA

S/No.		*Ushuru*	*Idadi*
1.	Ada ya kuandikishwa na usajili wa mhudumu mmoja	Tsh. 6,000/=	Kwa mwaka
2.	Ada ya kupima Afya kwa mtu mmoja	Tsh. 5,000/=	Kila baada ya miezi sita

SEHEMU E

USHURU WA MAZAO YA MALIASILI

S/No.	*Aina ya zao*	*Kiasi*	*Idadi*
1.	Mkaa	3500/=	Kwa kila gunia
2.	Usajili wa biashara ya mazao ya misitu.		Kwa mwaka
	(I) Mbao	200,000/=	
	(ii) Magogo	200,000/=	
	(iii) Nguzo	200,000/=	
	(iv) Fito	50,000/=	
	(v) Duka la bidhaa za misitu	200,000/=	
	(vi) Mkaa	200,000/=	
	(vii) Kuni	200,000/=	
	(viii) Furniture mart	200,000/=	
	(ix) Saw mill	400,000/=	
	(x) Fundi seremala	20,000/=	
	(xi) Madawa asili/kuranda/ kuchana mbao	100,000/=	
	(xii) Mashine ya kuchakata mbao.	300,000/=	

SEHEMU F

USHURU WA VIBAO VYA MATANGAZO

S/No.	*Aina ya Tangazo*	*Ushuru*	*Ukubwa*	*Muda*
1.	Matangazo yatakayobandikwa kwenye vibao na kuwekwa kando ya barabara kuu			
	(a) Yasiyotoa mwanga	Tsh. 3,000/=	Kila ft 1 ya mraba	Kwa mwaka
	(b) Yanayotoa mwanga	Tsh. 5,000/=	Kila ft 1 ya mraba	Kwa mwaka
2.	Matangazo ya biashara yanayobandikwa kwenye nyumba ya biashara			
	(a) Yasiyotoa mwanga	Tsh. 2,000/=	Kila ft 1 ya mraba	Kwa mwaka
	(b) Yanayotoa mwanga	Tsh. 2,500/=	Kila ft 1 ya mraba	Kwa mwaka
3.	Matangazo ya biashara yatakayobandikwa kwenye nyumba za makazi	Tsh. 1,000/=	Kila ft 1 ya mraba	Kwa mwaka
4.	Matangazo ya biashara kwa njia ya kipaza sauti	Tsh. 10,000/=	Kwa siku moja	Kwa siku

SEHEMU G

ADA YA KUCHANGIA UPIMAJI WA VIWANJA

S/No.	*Aina ya uwanja*	*Ada*
1.	Kiwanja kidogo (High Density)	Tsh. 40,000/=
2.	Kiwanja cha kati (Medium Density)	Tsh.50,000/=
3.	Kiwanja kikubwa (Low Density)	Tsh. 100,000/=
4.	Kiwanja kikubwa zaidi (super low density)	Tsh. 200,000/=

Tangazo la Serikali Na. 160 (linaendelea)

SEHEMU H

KIBALI CHA UJENZI

S/No.	*Aina ya jengo*	*Ushuru*
1.	Ghorofa 1	Tsh. 100,000/=
2.	Ghorofa 2 na kuendelea	Tsh. 120,000/=
3.	Nyumba za biashara	Tsh. 100,000/=
4.	Ghala au bohari	Tsh. 200,000/=
5.	Kituo cha mafuta	Tsh. 200,000/=
6.	Nyumba za makazi	Tsh. 20,000/=
7.	Nyumba za makazi na biashara	Tsh. 50,000/=
8.	Majengo mengine ambayo hayakutajwa hapo juu	Itategemea aina ya jengo
9.	Minara	Tsh. 1,500,000/=

SEHEMU I

ADA YA MABADILIKO YA JENGO LILILOPO/KIWANJA (ALTERATION)

S/No.	*Aina ya nyumba*	*Ushuru*
1.	Nyumba ya makazi	Tsh. 20,000/=
2.	Nyumba ya biashara	Tsh. 50,000/=
3.	Nyumba ya ghorofa	Tsh. 200,000/=
4.	Kiwanja, bohari, ghala	Tsh. 100,000/=
5.	Jengo lolote ambalo halijatajwa	Itategemea aina ya jengo

SEHEMU J

ADA YA KUMILIKI SLAHA

S/No.	*Aina ya ada*	*Kiwango*
1.	Kumiliki silaha (Gobore)	Tsh. 5,000/= Kwa mwaka

SEHEMU K

USHURU WA MADINI YA UJENZI

S/No.	*Aina ya madini*	*Ushuru* *Ujazo*
1.	Changarawe/Kokoto/Mawe/Kifusi/Mchanga	Tsh. 2000/= Kwa kila tripu moja ya lori/trekta

Tangazo la Serikali Na. 160 (linaendelea)

SEHEMU L

KODI YA PANGO MAJENGO NA VIBANDA VYA HALMASHAURI

S/No.	*Aina ya Jengo*	*Kodi ya pango*	*Muda*
1.	Vibanda ndani ya soko	Tsh.10,000/=	Kwa mwezi
2.	Vibanda nje ya soko	Tsh. 10,000/=	Kwa mwezi
3.	Vibanda ndani ya stendi	Tsh. 10,000/=	Kwa mwezi
4.	Vibanda nje ya stendi	Tsh. 10,000/=	Kwa mwezi
5.	Nyumba ya makazi ya Halmashauri (a) Nyumba	Tshs. 20,000/=	Kwa kila mpangaji

SEHEMU M

MAJENGO YA HALMASHAURI YALIYOKO SOKO KUU

S/No.	*Aina ya Jengo*	*Ushuru*
1.	Mabucha	40,000/= Kwa mwezi
2.	Maduka makubwa	50,000/= Kwa mwezi
3.	Vibanda vipya 12@ meza 8	5,000/= Kila meza kwa mwezi
4.	Meza 45 zilizo katikati ndani ya soko kuu	5,000/= Kila meza kwa mwezi

SEHEMU N

VYOO

S/No.	*Aina ya Jengo*	*Ushuru*
1.	Choo cha soko kuu	200/= Kwa kila kichwa
2.	Choo Stendi ya Somanda	200/= Kwa kila kichwa
3.	Huduma ya Bafu	500/= Kwa kila kichwa

SEHEMU O

USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO

S/No.	*Aina ya Zao*	*Ushuru*
1.	Mahindi	3% ya bei ya kununulia
2.	Mchele	3% ya bei ya kununulia
3.	Maharage	3% ya bei ya kununulia
4.	Karanga	3% ya bei ya kununulia
5.	Alizeti	3% ya bei ya kununulia
6.	Miwa	3% ya bei ya kununulia
7.	Mpunga	3% ya bei ya kununulia
8.	Dengu	3% ya bei ya kununulia
9.	Mbaazi	3% ya bei ya kununulia
10	Choroko	3% ya bei ya kununulia
11.	Mazao mengine ambayo hayakutajwa	3% ya bei ya kununulia

Tangazo la Serikali Na. 160 (linaendelea)

SEHEMU P

MAZAO YA BIASHARA

S/No.	*Aina ya Zao*	*Ushuru*
1.	Pamba	3% ya bei ya kununulia
2.	Katani (unela)	3% ya bei ya kununulia

SEHEMU Q

USHURU WA MASOKO/GULIO

S/No.	*Aina ya Bidhaa*	*USHURU*	*Muda*
1.	Nguo za mitumba	Tsh. 1,000/=	Kwa siku
2.	Nafaka rejareja	Tsh. 1,000/=	Kwa siku
3.	Madawa asili	Tsh. 1,000/=	Kwa siku
4.	Migahawa ndani ya soko	Tsh. 1,000/=	Kwa siku
5.	Samaki rejareja	Tsh. 1,000/=	Kwa siku
6.	Mboga za majani	Tsh. 500/=	Kwa siku
7.	Dagaa rejareja	Tsh. 1,000/=	Kwa siku
8.	Wauza vyungu	Tsh. 500/=	Kwa siku
9.	Miwa rejareja	Tsh. 1,000/=	Kwa siku
10.	Matunda/nyanya/vitunguu	Tsh. 500/=	Kwa siku
11.	Viatu rejareja	Tsh.1,000/=	Kwa siku
12.	Bidhaa nyinginezo	Tsh.1,000/=	Kwa siku
13.	Bidhaa zote zikiwemo za Kilimo siku ya gulio zitatozwa	Tsh.1,000/=	Kwa siku ya Gulio tu

SEHEMU R

USHURU WA MINADA

S/No.	*Aina ya jengo*	*Kodi ya pango*	*Muda*
1.	Ng'ombe	Tsh. 3,000/=	Kwa kila Ng'ombe
2.	Mbuzi/Kondoo	Tsh. 1,000/=	Kwa kila Mbuzi/Kondoo
3.	Nguruwe	Tsh. 1,000/=	Kwa kila Nguruwe

SEHEMU S

USHURU WA STANDI NA MAENGESHO

S/No.	*Aina ya gari*	*Ushuru*	*Idadi*
1.	Mabasi/malori	Tsh. 2,000/=	Kwa siku
2.	Hiace	Tsh. 1,000/=	Kwa siku
3.	Taxi	Tsh. 500/=	Kwa siku
4.	Bajaji	Tsh. 500/=	Kwa siku
5.	Magari ya watu Binafsi	Tsh. 500/=	Kwa siku

SEHEMU T

ADA YA USAJILI WA MAGARI YA BIASHARA/MIZIGO

S/No.	*Aina ya gari*	*Ada*	*Muda*
1.	Taxi	Tsh. 30,000/=	Kwa mwaka
2.	Pick ups	Tsh. 40,000/=	Kwa mwaka
3.	Trekta zinazofanya biashara	Tsh. 30,000/=	Kwa mwaka
4.	Lori za biashara tani 3.5 hadi 10	Tsh. 50,000/=	Kwa mwaka
5.	Lori za biashara tani 11 na kuendelea	Tsh. 80,000/=	Kwa mwaka

SEHEMU U

LESENI YA VILEO

S/No.		*Ushuru*	*Idadi*
1.	Wauzaji wa jumla	40,000/=	Kwa mwaka
2.	Baa	60,000/=	Kwa mwaka
3.	Grocery	30,000/=	Kwa mwaka

JEDWALI LA PILI

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya kifungu cha 7 cha sheria ndogo hizi)

Mimi ..... wa S.L.P. ..... ninaefanya biashara ya ..... katika eneo la .....lililopop ndani ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi. nakiri kuwa leo tarehe ..... Nilikiuka kifungu .....cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji wa Bariadi za mwaka 2012. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye sheria ndogo hizi iwapo mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 7 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini .....

Mbele yangu ..... (Jina)

Saini .....

Wadhifa .....

JEDWALI LA TATU

FOMU YA MAOMBI YA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI VYA BIASHARA AU VYOMBO VYA KUKODISHA

1. Jina kamili la mwombaji .....
2. Kazi ya mwombaji .....
3. Ainisho kamili la chombo cha usafiri .....
    a) Aina ya chombo .....
    b) Rangi .....
    c) Jina la mtengenezaji .....
    d) Aina ya modeli .....
    e) Namba ya injini .....
    f) Mwaka wa kuanza kutumika .....
    g) Idadi ya abiria inayoweza kubeba .....
    h) Namba ya leseni .....
4. Aini ya matumizi: (Tiki inayostahili)

a) Taksi ☐

b) Pick Ups ☐

c) Trecta ☐

d) Lori ☐

5. Kivuli cha usajili cha mwaka.

1. Kipo ☐ 2. Hakipo ☐

6. Namba ya usajili wa gari .....

7. Namba ya risiti ..... ya tarehe ..... ya Tsh .....

8. Namba ya gari ya ubavuni ..... (kwa daladala, taksi au pikipiki).

9. Jina la kituo cha maegesho .....

10. Iwapo mmiliki wa chombo cha usafiri cha biashara ataamua kuuza, kugawa au kuacha kazi ya biashara aliyoifanyia usajili chini ya Sheria ndogo iliyotajwa hapo juu, atalazimika kutaarifu halmashauri ya mji haraka iwezekanavyo.

Nathibitisha kuwa taarifa nilizozitoa hapo juu ni sahihi na kweli kwa utimilifu wa akili na imani yangu.

Sahihi ya mwombaji: .....

Tarehe: .....

Kwa matumizi ya ofisi tu.

1. Sahihi ya mwandisi wa Halmashauri .....

Tarehe: .....

2. Sahihi ya Mkurugenzi .....

Tarehe: .....

Tangazo la Serikali Na. 160 (linaendelea)

Nembo ya Halmashauri ya Mji umebandikwa kwenye Hati Rasmi kwa kuzingatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 11 mwezi Desemba mwaka 2012 na Nembo hiyo imebandikwa mbele ya:-.

ERICA MUSSIKA,
Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji
Bariadi

L.S.

ROBERT LWEYO MGATA,
Mwenyekiti
Halmashauri ya Mji Bariadi

NAKUBALI,

MHE. MIZENGO P. PINDA (MB.),
Waziri Mkuu

15 Machi, 2013.

TANGAZO LA SERIKALI NA.161 la tarehe 07/06/2013

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA 288)

SHERIA NDOGO

(Imetungwa Chini ya Kifungu cha 58).

HATI RASMI YA UANZISHAJI WA BODI YA HUDUMA ZA AFYA YA HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI, 2013

Jina na tarehe kutumika

1. Hati hii itajulikana kama Hati Rasmi ya uanzishaji wa Bodi za Huduma ya Afya ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi ya mwaka 2012 na itaanza kutumika baada ya kutangazwa katika *Gazeti* la serikali.

Eneo la matumizi

2. Hati hii itatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi.

Tafsiri

3. Katika Hati hii isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:-

"Bodi" maana yake ni bodi ya huduma za afya ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi iliyoundwa chini ya kifungu cha 4(1) cha Hati Rasmi hii;

"Chombo cha afya" maana yake ni pamoja na Hospitali, kituo cha afya, kliniki za madawa na meno, zahanati, duka la madawa, maabara ya afya, kituo cha uchunguzi, nyumba za kujifungulia na nyumba ya wagonjwa ni pamoja na vyombo vingine vilivyoundwa na kupangwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za afya;

"Chombo cha afya binafsi" maana yake ni chombo cha afya kinachomilikiwa na kuongozwa na mtu binafsi au kampuni kwa faida..

"Chombo cha afya cha umma" maana yake ni chombo cha afya kinachomilikiwa na kuongozwa na serikali kwa mahitaji ya watu;

"Chombo cha afya cha shirika lisilokuwa la kiserikali" maana yake ni chombo cha afya kinachomilikiwa, fadhiliwa na au kinachoongozwa na shirika au jumuiya inayoongoza huduma binafsi bila faida, na inayofanya kazi.

Tangazo la Serikali Na. 161 (linaendelea)

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Bariadi;

"Hospitali" maana yake ni Hospitali iliyoanzishwa katika eneo la Halmashauri yenye uwezo wa kusimamia huduma zote za afya;

"Kamati ya Uchumi Afya na Elimu ya Halmashauri" maana yake ni Kamati iliyoundwa chini ya kifungu cha 47(1) cha Sura Na. 288.

"Kamati ya kituo cha afya" maana yake ni kamati iliyoundwa chini ya kifungu cha 26 cha Hati hii;

"Kamati za Zahanati" maana yake ni Timu ya wataalam wanaoongoza huduma za afya ndani ya Zahanati.

"Kamati ya Maendeleo ya kata" (WDC) maana yake ni kamati iliyoundwa chini ya kifungu cha 16 cha sura ya 288;

"Kamati ya Afya ya Kata" maana yake ni kamati iliyoundwa chini ya kifungu cha 34 cha Hati hii;

"Kamati ya wataalam wa Hospitali" maana yake ni kamati iliyoundwa chini ya kifungu cha 17 na Hati hii;

"Kaya" maana yake ni:-

(a) mama, baba, watoto wenye umri chini ya miaka kumi na nne;

(b) Mwanachama yeyote aliyefikisha umri wa miaka kumi na nane au zaidi na awe na mtoto au bila mtoto mwenye umri wa miaka kumi na nane;

(c) Taasisi yoyote.

"Kituo cha afya" maana yake ni chombo cha afya kinachotoa huduma za afya kwa wagonjwa wote wa nje na ndani pamoja na mama na mtoto na wagonjwa wa ndani wasiozidi vitanda 15;

'Mfuko wa Afya ya Jamii" (CHF) maana yake ni mfuko ulioundwa na kuungwa kama mpango wa bima ya hiari ambapo kaya zitakuwa zikilipia huduma za afya kuwawezesha wanachama na familia zao kupata matibabu kutoka kwa mtoaji fulani kwa kipindi fulani;

"Mganga Mkuu wa Halmashauri" Maana yake ni mganga Mtendaji mkuu wa shughuli zote za huduma za afya ndani ya Halmashauri;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), (Sura 288);

"Taasisi" maana yake ni pamoja na shule au vyuo vilivyosajiliwa kwa mujibu wa sheria iliyokubaliwa na kuidhinishwa na Bodi;

"Timu ya wataalam wa Afya Mkoa" (RHMT) maana yake ni timu ya wataalam wa afya wakuu wanaoongoza huduma za afya mkoani;

"Timu ya watalam wa afya wa Halmashauri" (CHMT) maana yake ni timu ya wataalam wakuu wa Halmashauri iliyoundwa chini ya kifungu cha 14 cha Hati hii;

"Timu ya wataalam wa kituo cha Afya" maana yake ni timu ya wakuu wa idara au vituo vya Afya kama ilivyo katika mwongozo wa vifaa vya afya na Waziri wa Afya ya mwaka 1996;

"Timu ya wataalam wa Hospitali" maana yake ni timu ya wataalam wakuu wanaoongoza huduma za afya Hospitalini;

"Zahanati" maana yake ni vifaaa vya afya vinavyotoa huduma za afya kwa wagonjwa pamoja na huduma za afya kwa mama na mtoto na huduma za maabara. inaweza kutoa huduma za uchunguzi kwa wagonjwa walioteuliwa. kiwango cha juu cha vitanda kwa uchunguzi ni vinne;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa.

Bodi

4.—(1) Kutakuwa na Bodi ambayo itajulikana kama Bodi ya Huduma za afya ya Halmashauri.

(2) Ofisi za Bodi zitakuwa katika eneo la Halmashauri.

Wajumbe wa Mfuko wa Bodi

5.—(1) Bodi itaundwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Wawakilishi wanne watumiaji huduma za afya kati yao wawili ni lazima wawe ni wanawake.

(b) Mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za afya binafsi bila faida na mwakilishi mmoja kutoka huduma za afya binafsi kwa faida waliochaguliwa na Halmashauri kutoka vituo vya kutolea huduma za afya na Bodi.

(c) mwenyekiti wa kamati ya uchumi, afya na elimu ya Halmashauri.

(d) Afisa Mipango wa Halmashauri.

(e) Mganga Mkuu wa Halmashauri ambae atakuwa Katibu wa Bodi.

(f) Afisa Mkuu kutoka Hospitali ya Halmashauri.

(g) Mwakilishi mmoja kutoka Timu ya wataalam wa afya Mkoa.

Tangazo la Serikali Na. 161 (linaendelea)

(2) Mwenyekiti atachaguliwa na wajumbe chini ya aya (a), (b), (c) ya kifungu hiki.

(3) Wajumbe waliotajwa katika aya (a) (b) na (c) mbali na wajumbe waliotajwa katika aya (d), (e), (f) na (g) za kifungu kidogo cha (1) watakuwa na haki ya kupiga kura katika maamuzi ya Bodi.

Sifa za mjumbe wa Bodi

6.—(1) Mjumbe wa Bodi atakuwa na sifa zifuatazo:-

(a) awe raia wa Tanzania na suala la uraia halitahusisha uwakilishi wa vyama visivyokuwa vya kiserikali na hiari.

(b) awe na umri si chini ya miaka ishirini na tano na awe mwenye mwili na akili timamu.

(c) awe amemaliza elimu ya Sekondari katika shule iliyosajiliwa.

(2) Isipokuwa kwa Mwenyekiti wa Halmashauri wajumbe wa Kamati za Uchumi, Afya na Elimu katika Bodi ya afya ya Halmashauri hawatashiriki nyadhifa zozote za kisiasa.

(3) Bodi itafunguliwa na Halmashauri mbele ya Mkuu wa Wilaya.

Vikao vya Bodi

7.—(1) Kwa kuzingatia kanuni za kifungu kidogo cha 2 cha kifungu hiki, Bodi itakuwa inakutana kwa kikao cha kawaida kila robo ya mwaka wa kalenda na mikutano yote ya Bodi itaitishwa na katibu.

(2) Katibu ataitisha kikao maalum kitakachokuwa cha kawaida cha Bodi kwa maombi yaliyoandikwa na kusainiwa na wajumbe wa Bodi wasiopungua theluthi moja na pale itakapohitajika.

Akidi ya Kikao

8.—(1) Theluthi mbili ya jumla ya wajumbe wote wa Bodi watatengeneza akidi katika kila mkutano wa bodi.

(2) Uamuzi wa wajumbe wengi waliopo na waliopiga kura katika mkutano wa bodi utachukuliwa kama uamuzi wa Bodi.

(3) Pindi mwenyekiti wa kawaida atakapokuwa hayupo mwenyekiti mwingine wa muda atachaguliwa chini ya kifungu cha 5 kifungu kidogo cha 2 cha Hati hii.

(4) Kila mjumbe wa Bodi atakuwa na kura moja na pindi kura zitakapokuwa sawa katika upigaji kura, Mwenyekiti wa mkutano atapiga kura nyingine upande wowote zaidi ya ule aliyoupigia katika upande ule aliouchagua au kura ya turufu.

(5) Kura ya siri itakuwa inatumika katika mikutano yote ya Bodi.

Kazi za Bodi

9. Majukumu, kazi na wajibu wa Bodi itakuwa kama ifuatavyo:-

(a) kuhakikisha kwamba watu wanapata huduma ya afya iliyo bora, yenye kinga, inayotibu na inayokarabati iliyosahihi na inayowezekana.

(b) kujadili, kukabili mipango ya afya, bajeti na kuzipeleka kwa Halmashauri na kuzipitisha.

(c) kupokea, kuchambua na Kupitisha ripoti za utekelezaji wa timu ya wataalam wa afya wa Halmashauri.

(d) kutambua, kukusanya na kutafuta vyanzo vya fedha kwa uendeshaji wa huduma ya afya ya Halmashauri.

(e) kukusanya vyanzo vitoshavyo ambavyo vitahakikisha ukamilifu, Usanifu na usawa mbele ya huduma za afya ndani ya Halmashauri.

(f) kusaidia timu ya wataalam wa afya wa Halmashauri katika kuongoza na kusimamia huduma ya afya.

(g) kuandaa na kupendekeza juu ya mpango mpana wa afya na bajeti kwa kamati ya Elimu ya Afya na Maji.

(h) kuboresha miundo mbinu endelevu ya afya na njia za usambazaji.

(i) kuendeleza, kusimamia na kuongoza huduma za afya ndani ya Halmashauri.

(j) kushauri, kupendekeza juu ya mafunzo kwa waajiri, uteuzi, ajira na maendeleo ya Halmashauri.

(k) kujadili juu ya pendekezo la mchango kwa mwaka kutoka kamati ya afya ya kata na kupeleka pendekezo hilo katika Halmashauri kutoka mfumo wa afya ya jamii.

(l) Kushirikiana na Kamati za Afya za Halmashauri.

Uhusiano wa Bodi na Vyombo vingine

10.—(1) Uhusiano wa Bodi na jamii, wadau na mamlaka nyingine utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Timu ya wataalam wa afya ya Halmashauri itakuwa na muundo wa kiufundi katika kutekeleza maamuzi yaliyopitishwa na Bodi.

(b) kwa kuheshimu kamati ya Uchumi, Afya na Elimu;

(i) mipango na ripoti zote za maendeleo ya Bodi zitapitia katika kamati hii ili kupata ushirikiano.

(ii) Bodi katika kutekeleza mwingiliano ambao utahitaji, nguvu za pamoja itatafuta ushirikiano wa karibu na sekta nyingine.

(iii) Bodi itahakikisha kuwa jamii inashirikishwa kikamilifu katika kutambua matatizo, kuweka kipaumbele, kupanga, kuchangia, kufuatilia na kutathimini utoaji huduma za afya.

(iv) Bodi itaendesha shughuli zake kwa utaratibu wa uwazi na ambao utakuza ufanisi kwa Halmashauri na vyombo vyake vingine vya utendaji bila Halmashauri kuingilia ushuru wa Bodi.

(c) kwa upande wa vyama visivyo vya kiserikali, wachangiaji binafsi na wafadhili;

(i) Wajumbe wanaowakilisha vikundi vya hiari, vyama visivyo vya kiserikali na wachangiaji binafsi na wafadhili ndani ya Bodi kutaleta ushusiano muzuri baina yao.

(ii) Bodi itahitaji uhakika kutoka kwa Timu ya wataalam wa afya wa Halmashauri ambapo itakuwa ni chombo cha kitaalam katika utekelezaji wa maamuzi ya Bodi.

(iii) Bodi itafute pesa kutoka vyanzo vya pesa mbalimbali vikiwemo vya Halmashauri, vikundi vya hiari, jamii na wafadhili.

(d) Timu ya wataalam wa afya wa Mkoa itatoa msaada wa kiufundi na ushauri.

(2) Majukumu ya Mawaziri wanaohusika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Afya yatakuwa kutunga sera, kanuni za usimamizi na kusimamia kazi za Bodi ya Huduma za afya ya Halmashauri.

Vyanzo vya mapato

11.—(1) Vyanzo vya Mapato vya Bodi vitakuwa:-

(a) michango ya jamii.

(b) mfuko wa afya ya jamii.

(c) kuchangia gharama na ada kwa matumizi ya vifaa.

(d) makusanyo ya mapato ya Halmashauri.

(e) wafadhili na washirika.

(f) ruzuku kutoka serikali kuu.

(g) vyanzo vingine.

(2) Kwa madhumuni ya kuendeleza mfuko wa afya ya jamii kutafunguliwa na kuendelezwa akaunti ya Benki kwa jina la Mfuko wa Afya ya Jamii ya Mji Bariadi.

(3) Akaunti ya mfuko wa afya ya jamii Mji wa Bariadi itapata mapato makubwa kutoka:-

(a) mauzo ya kadi za mfuko wa afya ya Halmashauri.

(b) makusanyo ya ada kutokana na matumizi ya vifaa vya afya vya Halmashauri.

(c) vyanzo vingine vya mapato vilivyotajwa katika kifungo cha 11 (1) hapo juu.

waweka saini wa akaunti ya mapato haya watakuwa kama walivyoonyeshwa katika Sheria Ndogo iliyoanzisha mfuko wa afya ya jamii.

(4) Halmashauri itawateua wahasibu wawili ambao wataangalia akaunti ya afya chini ya mganga mkuu wa Halmashauri.

(5) Mganga Mkuu wa Halmashauri ndiyo ataanzisha malipo yote.

(6) Akaunti zote mbili zitakaguliwa, kufuata kanuni za Serikali katika ukaguzi wa akaunti za Halmashauri.

(7) Sheria Ndogo za mfuko wa afya ya jamii zitatengenezwa kwa madhumuni ya kuongoza kazi za Bodi za huduma ya afya zilizoundwa chini ya Hati hii.

12. Bodi itawajibika kwa Halmashauri ambapo:-

Wajibu wa Bodi kwa Halmashauri

(a) mipango ya afya ya Halmashauri, kila robo mwaka na ufundi na taarifa za fedha za mwaka zitapitishwa na kamati ya Uchumi, Afya na Elimu na kuhakikiwa na Baraza la Madiwani.

(b) Bodi itafanya kazi zake katika njia ambayo itaongeza ufanisi wa Halmashauri na vyombo vyake.

13.—(1) Iwapo Bodi imeshindwa kukamilisha majukumu iliyopangiwa kama inavyoonyeshwa kwenye Hati hii, Halmashauri itavunja Bodi na kupanga uteuzi wa haraka.

(2) Iwapo Bodi inapovunjwa, wajumbe wote watapoteza nafasi zao.

(3) Kwa kipindi ambacho hakutakuwa na Bodi ya Afya ya Halmashauri, Halmashauri itaipa uweza timu ya wataalam wa Afya wa Halmashauri uwezo ambao Bodi ilikuwa nao.

14. Kutakuwa na Timu ya Wataalam wa Afya wa Halmashauri kama ilivyo katika muundo wa utawala wa wizara ya afya katika maelezo ya majukumu, madhumuni na kazi za Timu ya Wataalam wa afya wa Mkoa (RHMT), Timu ya wataalam wa afya wa Halmashauri ya Mji (CHMTS), na timu nyingine za wataalam wa afya zinazohusiano na Bodi ya huduma ya afya za Halmashauri (CHSBS).

Timu ya uendeshaji huduma za afya za Halmashauri

15. Timu ya wataalam wa afya wa Halmashauri itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mganga mkuu.

(b) Katibu wa afya.

(c) Muuguzi mkuu.

(d) Bwana afya.

(e) Mfamasia.

(f) Mtaalam wa maabara.

(g) Mganga wa meno.

Madhumuni ya kkazi za timu ya wataalam

16. Madhumuni na kazi za Timu ya wataalam yatakuwa ni:-

(a) kuandaa mipango kabambe ya afya pamoja na mahitaji ya afya na mwongozo wa Taifa wa mpango wa afya;

(b) kuhakikisha kwamba kazi za afya zinafanywa na hospitali, vituo vya afya, zahanati na vinamiliki vifaa kutokana na mpango huo kabambe wa afya.

(c) kuhakikisha upatikanaji wa usafiri, na madawa, sindano, vifaa vya afya na kudhibiti njia za kuzuia matatizo;

(d) kupambana na magonjwa ya milipuko, dharura na kuweka mpango wa kudhibiti na njia za kutatua matatizo hayo.

(e) kutoa msaada wa kiusimamizi wa afya ukiwa na viwango vya kimataifa;

(f) kuhakikisha kuwa ubora wa huduma za jamii unatolea ukiwa na viwango vya kimataifa.

(g) kuhakikisha kwamba sheria za afya, kanuni na miiko ya kitaaluma, na kanuni za kinidhamu zinafuatwa ndani ya Halmashauri.

(h) kuhakikisha kwamba ukusanyaji wa taarifa, uchambuzi, matumizi na utoaji wa taarifa unatumiwa na wafanyakazi katika mpango wa afya na kutekeleza miingiliano.

(i) kutambua maeneo ya kupewa kipaumbele, kuunganisha na kufanya utafiti ndani ya Halmashauri;

(j) kukusanya na kuchambua ripoti za fedha kila robo mwaka na za ufundi kila mwaka na kuzipeleka katika Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri na timu ya wataalam wa Afya wa Mkoa;

(k) kuandaa mikutano ya wahusika na watendaji wote wa afya katika Halmashauri ili kutambua na kuunganisha kazi zote za afya;

(l) kuandaa na kusaidia huduma za afya zisizofikiwa.

(m) kusimamia na kuchanganua utekelezaji wa kazi za afya za Halmashauri.

17. Katika kila Hospitali kutakuwepo na kamati ya wataalam wa Hospitali itakayokuwa chini ya uongozi na usimamizi wa Halmashauri.

Wajumbe wa Kamati ya wataalam wa Hospitali

18. —(1) Kamati ya wataalam wa Hospitali itaundwa na:-

(a) wajumbe wa kuchaguliwa;

(i) Wajumbe watatu wenye tabia nzuri waliochaguliwa kutoka katika wanachama wanaotumia huduma za afya za jamii au wajumbe waliosajiliwa kupokea huduma kutoka Hospitali.

(ii) Wajumbe wawili walioteuliwa na kuthibitishwa na timu ya wataalam wa afya ya Halmashauri kutoka katika wanachama wa kamati za vituo vya afya na zahanati ndani ya eneo ambalo Halmashauri ina mamlaka.

(iii) Mjumbe mmoja aliyethibitishwa na Halmashauri, vituo vya ndani vinavyotoa huduma katika eneo lote la Halmashauri.

(iv) Mjumbe mmoja aliyethibitishwa na Halmashauri kutoka watoa huduma za afya (Jamii) binafsi kwa faida ndani ya eneo la Halmashauri.

(b) Wajumbe wa kuteuliwa:-

(i) Mjumbe mmoja kutoka Bodi ya huduma za afya ya Halmashauri.

(ii) Mganga mkuu wa Hospitali ambaye atakuwa Katibu.

(iii) Mwakilishi mmoja kutoka katika ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri.

(2) Theluthi moja ya wajumbe wote watakuwa wanawake.

(3) mwenyekiti wa kamati ya wataalam wa Hospitali atachaguliwa na wajumbe waliochaguliwa na kamati.

(4) kamati inaweza kumkaribisha mtu yeyote kutoa utaalam na msaada mwingine lakini mtu huyo hatakuwa mtoa maamuzi ya mwisho ya kamati.

Sifa za wajumbe wa kamati ya Wataalam wa Hospitali

19. Wajumbe wa kamati ya wataalam wa Hospitali watakuwa na sifa zifuatazo:-

(a) awe raia wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na suala la uraia halitahusiana na uwakilishi wa vyama visivyo vya Kiserikali (NGOs) au vyama vya hiari.

(b) awe na umri wa miaka 21 na zaidi.

(c) awe na Elimu ya Sekondari au zaidi.

(d) hana cheo chochote katika masuala ya Siasa.

Vikao vya Kamati ya Usimamizi ya Hospitali

20.—(1) Kamati ya Hospitali itakuwa na vikao vya kawaida kwa Uendeshaji wa shughuli zake walau mara moja kwa mwezi.

(2) Mwenyekiti wa kamati baada ya kushauriana na katibu anaweza kuitisha kikao maalum au kisichokuwa cha kawaida kwa kipindi kile atakapoona yafaa.

(3) Taarifa ya kikao chochote itapelekwa kwa wajumbe sio chini ya siku mbili kabla ya tarehe iliyoteuliwa na kikao ikiwaeleza wajumbe kwa maandishi mahali, tarehe na muda wa kikao na shughuli itakayofanyika katika kikao hicho.

Kazi za Kamati ya wataalam wa Hospitali

21. Kazi, madhumuni na wajibu wa kamati ya wataalam wa Hospitali itakuwa kama ifuatavyo:-

(a) kuangalia usimamizi sahihi wa vifaa vya Hospitali.

(b) kupokea na kujadili utekelezaji wa taarifa zilizoandaliwa na timu ya wataalam wa Hospitali na bajeti na kuzipeleka katika

Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri.

(c) kupokea na kujadili utekelezaji wa taarifa zilizoandaliwa na Timu ya wataalam wa Hospitali.

(d) kutambua, kukusanya na kutafuta fedha kwa huduma za Hospitali.

(e) kuwasiliana na kamati nyingine na washirika wengine katika kutoa na kuboresha afya.

(f) kuhamasisha jamii katika operation za Hospitali na mipango ya maendeleo.

(g) kuweka mapendekezo katika ajira, mafunzo na motisha kwa watu mbalimbali.

Uwajibikaji na utoaji taarifa

22. Kamati ya wataalam wa Hospitali itawajibika kwa Halmashauri.

Uhusiano wa kamati na kamati nyingine

23. Kwa lengo la uongozi bora kamati ya wataalam wa Hospitali utawasiliana na kamati nyingine za afya au watoa huduma za afya kutengeneza mwingiliano wa utoaji wa huduma za afya ndani ya muundo ulioanzishwa.

Vyanzo na usimamizi wa mapato

24.—(1) vyanzo vya mapato vya kamati ya wataalam wa Hospitali vitakuwa:-

(a) kiasi kile ambacho Hospitali ya Halmashauri itakuwa imepangiwa na Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri.

(b) ada na matumizi ya Hospitali au sehemu zake kama zitakavyokuwa zimepangwa na Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri.

(c) kiwango kile kitakachopokelewa kama ruzuku au punguzo, mchango kutoka Halmashauri, serikali kuu, taasisi na watu binafsi.

(d) pesa zozote ambazo zitakuwa zimepokelewa kisheria na Bodi kutoka vyanzo vingine ambavyo havijatajwa katika Hati hii.

(2) Kutakuwa na akaunti moja ya Hospitali ambayo itafuata kanuni zilizopo za fedha za Serikali za Mitaa.

(3) Mganga Mkuu ataanzisha na kulipa malipo yote ya shughuli za Hospitali.

Tangazo la Serikali Na. 161 (linaendelea)

Kuvunjwa kwa kamati

25.—(1) Endapo kamati ya wataalam wa Hospitali itashindwa kutimiza malengo yake, Halmashauri itaionya au kuivunja na kupanga uteuzi wake ndani ya kipindi cha miezi mitatu.

(2) Pale kamati ya wataalam wa Hospitali itakapokuwa imevunjwa, wajumbe wote watapoteza nafasi zao

(3) kwa kipindi chote ambacho hakutakuwa na kamati ya wataalam wa Hospitali Halmashauri itaipa uwezo huo wa kamati ya wataalam wa Hospitali timu ya wataalam wa Hospitali.

Kamati ya Kituo cha afya

26.—(1) Kutaanzishwa katika kila kituo cha afya kamati ya kituo cha afya kamati ya kituo cha afya ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) wajumbe watatu wenye tabia nzuri waliochaguliwa kutoka katika wanachama wanaotumia huduma za afya za jamii au wajumbe waliosajiliwa kupokea huduma kutoka Hospitalini.

(b) mjumbe mmoja aliyeteuliwa na vyama visivyo vya kiserikali (NGOs) vinavyotoa huduma za afya katika eneo.

(c) mkuu wa kituo cha afya ambaye atakuwa katibu.

(d) mjumbe mmoja aliyeteuliwa kutoka sekta binafsi inayotoa huduma ya afya bila faida katika eneo.

(e) wajumbe wawili kutoka kamati za zahanati ambao watachaguliwa kila mwaka.

(f) mjumbe mmoja kutoka katika kamati za maendeleo za kata (WDC) watakaochaguliwa kila mwaka.

(2) Kamati ya kituo cha afya inaweza kumkaribisha mtu yeyote kutoka utaalam na msaada mwingine, lakini mtu huyo hatakuwa mtoa maamuzi ya mwisho ya kamati.

(3) Walau thelathini moja ya wajumbe wote watakuwa wanawake.

Sifa za mjumbe wa kamati ya kituo cha afya

27. Mtu atateuliwa kuwa mjumbe wa kamati ya kituo cha afya akiwa na sifa zifuatazo:-

(a) awe raia wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na suala la uraia halitahusiana na uwakilishi wa vyama visivyo vya kiserikali (NGOs) au vyama vya hiari.

(b) awe na umri wa miaka 21 na sio zaidi ya miaka 65.

(c) ni mkazi wa eneo ambalo Halmashauri ina mamlaka.

(d) anaweza kusoma na kuandika Kiswahili.

(e) hana cheo chochote katika masuala ya siasa.

Vikao vya kamati

28.—(1) Kamati itakuwa na vikao vya kawaida kwa uendeshaji wa shughuli zake walau mara moja kila baada ya miezi mitatu.

(2) Mwenyekiti wa kamati ataitisha kikao maalumu au kisicho cha kawaida cha kamati na kuelekeza madhumuni ya kikao hicho baada ya kupokea maombi ya maandishi yaliyosainiwa na wajumbe wa kamati wasiopungua theluthi moja.

(3) Katibu atamwarifu kila mjumbe kwa maandishi juu ya sehemu, siku na muda wa kikao na shughuli inayotakiwa ifanye kwa kipindi kisichopungua masaa 24 kabla ya muda wa kikao.

Kazi za kamati ya kituo cha afya

29. Kamati ya kikao cha afya itakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji zilizotayarishwa na timu ya wataalam kutoka kituo cha afya.

(b) kutambua na kutafuta pesa kwa uendeshaji wa kituo cha afya.

(c) kuwasiliana na Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri na washiriki wengine katika utoaji na uboreshaji wa huduma katika eneo.

(d) kufanya miundo ya afya endelevu na usambazaji wa madawa na ubadilishaji wa vifaa na watumishi unaowezekana.

(e) kushauri na kupendekeza kwa Bodi ya huduma za afya ya Halmashauri katika maendeleo ya watu juu ya kuajiri, kutoa motisha ya mafunzo katika kituo cha afya.

Kuwajibika kwa kamati

30. Kamati ya kituo cha afya itawajibika kwa Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri

Vyanzo vya mapato

31.—(1) Fedha na vyanzo vya mapato ya kituo cha afya vitakuwa vifuatavyo:-

(a) michango ya jamii.

(b) wafadhili au michango ya washirika.

(c) ruzuku kutoka Serikalini

(d) ruzuku kutoka Halmashauri

(e) chanzo chochote halali

(2) Fedha zitawekwa katika akaunti na itasimamiwa na kuongozwa na mganga mkuu wa Halmashauri.

Tangazo la Serikali Na. 161 (linaendelea)

32.—(1) Katika ufanyaji wake kazi za kamati ya kituo cha afya:-

(a) itahakikisha matakwa ya jamii yanatekelezwa.

(b) itatafuta fedha kutoka vyanzo mbambali.

(c) itatunza na kuweka kumbukumbu za wachangiaji wa mfuko wa afya.

(d) itaendeleza na kuimarisha ushirika (partinership) kwa mahusiano, uunganishaji na mwingiliano na sekta nyingine katika eneo.

(e) itahakikisha kwamba kamati ya kituo cha afya inawakilishwa katika Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri.

(2) Timu ya wataalam wa afya wa Halmashauri itatoa ushauri wa kiufundi kwa timu ya wataalam wa kituo cha afya.

(3) Kamati za kituo cha afya zitawasilisha taarifa za maendeleo kwa Bodi ya huduma ya afya ya Halmashauri kila robo mwaka, nusu na mwaka.

Kuvunjwa kwa kamati

33.—(1) Endapo kamati ya kituo cha afya itashindwa kutimiza malengo yake kama yalivyoonyeshwa katika Hati hii, Halmashauri itavunja Bodi na kupanga uteuzi wake ndani ya kipindi cha miezi mitatu.

(2) Kwa kipindi chote ambacho hakutakuwa na kamati ya wataalam wa kituo cha afya, Halmashauri itaipa uwezo wa kamati ya wataalam wa kituo cha afya Timu ya wataalam wa kituo cha afya.

Kamati ya afya ya kata

34. Kutakuwa na Kamati ya Afya ya Kata.

35.—(1) Kamati ya afya ya kata itaundwa na:-

(a) diwani wa kata husika

(b) afisa mtendaji wa kata.

(c) Mwalimu Mkuu mmoja katoka shule ya msingi iliyopo ndani ya kata ambaye atateuliwa na kamati ya maendeleo ya kata.

(d) Wajumbe wawili kutoka katika jamii moja kati ya hao atakuwa Mwanamke.

(e) mganga au msaidizi wa mganga mfawidhi wa chombo cha afya, ambaye atakuwa katibu wa kamati.

(f) mjumbe mmoja aliyeteuliwa na kamati ya maendeleo ya kata kutokana na watu waliopendekezwa na vijiji ndani ya eneo

la kata.

(g) mjumbe mmoja kutoka jamii aliyeteuliwa na kamati ya maendeleo ya kata.

(2) Kama kamati ya afya ya kata itashindwa kutimiza malengo yake Halmashauri itaionya au kuvunja na kupanga uchaguzi wa haraka na uteuzi ndani ya kipindi cha miezi mitatu.

Sifa za mwana-chama wa kamati ya Afya ya kata

36. Mtu atateuliwa kuwa mwanachama wa kamati ya afya ya kata akiwa ana sifa zifuatazo:-

(a) awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) awe ana umri wa miaka 21 na sio zaidi ya 65.

(c) anaweza kusoma na kuandika kiswahili.

37. Kamati ya afya ya kata itakuwa na kazi zifuatazo;

(a) kuhamasisha jamii kuwa na wanachama wa mfuko wa afya ya jamii

(b) kuandaa orodha ya wanachama na kusajili kwa wakati ipasavyo.

(c) kusimamia wakusanyaji wa mfuko wa afya ya jamii.

(d) kuhakikisha usawa wa ukusanyaji na matumizi ya mapato.

(e) kupitia operasheni za mfuko wa afya ya jamii, kupendekeza na kuhakikisha kama itakavyokuwa inafaa.

(f) kuanzsha na kuunganisha mipango kabambe ya afya ya jamii

(g) kufanya mikutano ya wanachama wa mfuko wa afya ya jamii

(h) kupendekeza kwa Halmashauri michango ya mwaka kwa wanachama wa mfuko.

Kamati ya Zahanati

38. Kutakuwa na kamati itakayojulikana kama Kamati ya Zahanati.

39. Kamati ya zahanati itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Wajumbe wa kuchaguliwa watakaokuwa wapiga kura kama ifuatavyo:-

(i) Wajummbe watatu kutoka katika jamii inayotumia Zahanati.

(ii) Mwakilishi mmoja kutoka katika vyama visivyo vya Kiserikali vinavyotoa huduma ya afya bila faida.

(iii) Mwakilishi mmoja kutoka katika watoa huduma ya afya binafsi kwa faida.

(b) Wawakilishi wanachama wasio wapiga kura kama ifutavyo:-

(i) mwakilishi mmoja kutoka kamati ya maendeleo ya kata atakayeteuliwa kwa mwaka.

(ii) Mwakilishi mmoja kutoka kamati za Serikali ya kijiji atakayeteuliwa kwa mwaka.

(iii) Mkuu wa zahanati wambaye atakuwa katibu

Vikao vya Kamati ya Zahanati

40.—(1) Kamati ya Zahanati itakutana kila robo mwaka, lakini inaweza kuitisha kikao cha dharura pale itakapohitajika.

(2) Asilimia 50% ya wajumbe waliochaguliwa pamoja na mwenyekiti na katibu watatengeneza akidi inayotakiwa kwa kikao cha kamati Zahanati.

Sifa za Mjumbe wa Kamati ya zahanati

41. Mtu atakuwa mjumbe wa kamati ya zahanati akiwa na sifa zifuatazo:-

(a) ana umri wa miaka 21 na zaidi, na anaweza kusoma na kuandika kiswahili au kiingereza.

(b) raia wa Tanzania na ni mkazi wa eneo husika. Hata hivyo suala la Uraia halitahusisha wawakilishi binafsi au vyama visivyo vya Kiserikali.

(c) hana cheo chochote cha kisiasa

(d) ni mwenye akili timamu

(e) hakuwahi kukutwa na kosa lolote la jinai.

Kazi za kamati ya zahanati

42. Kamati ya zahanati itakuwa na madhumuni na kazi zifuatazo:-

(a) kuhakikisha kwamba jamii katika eneo la mamlaka yake inapata Huduma ya afya inayowezekana na sahihi.

(b) kupokea, kujadili nakupitisha mipango na bajeti ya zahanati

(c) kujadili utekelezaji wa taarifa zilizoandaliwa na timu ya wataalam wa Zahanati

(d) kutambua na kukusanya fedha kwa uendeshaji wa zahanati.

(e) kuwasiliana na Bodi na washirika katika utoaji na uboreshaji wa afya.

(f) kufanya miundo mbinu ya afya endelevu na usambazaji na uboreshwaji wa watumishi unaowezekana.

(g) kusaidia na kuwezesha Timu ya wataalam wa Zahanati katika mpango na usimamizi wa afya ya jamii katika eneo na ndani ya mpango wa maendeleo wa kata.

43. Kamati ya Zahanati kwa madhumuni ya uongozi mzuri:-

(a) itahakikisha jamii inawakilishwa na matakwa yao yanatekelezwa.

(b) itapokea na kuendana na ushauri wa afya wa Halmashauri.

(c) itawasilisha taarifa za robo mwaka na za mwaka kwa Bodi ya Huduma ya afya ya Halmashauri.

(d) itahakikisha kwamba zahanati husika zinakumbukwa na kamati ya kituo cha afya kwa uwakilishi wa mzunguko.

(e) inaendeleza na kuimarisha ushirika (Partinership kwa mahusiano) uunganishaji na mwingiliano na sekta nyingine katika eneo.

Vyanzo vya fedha za Kamati ya Zahanati

44. Vyanzo vya fedha kwa kamati ya Zahanati vitahusisha lakini siyo Pekee kwa vifuatavyo:-

(a) michango ya jamii.

(b) mfuko wa afya ya jamii.

(c) mfuko wa Halmashauri.

(d) fedha kutoka kwa wafadhili na washirika (patners)

(e) serikali kuu.

(f) vyanzo vingine halali

Muda wa kukaa Madara-kani

45. (a) Wajumbe wote wa Bodi na kamati zote za afya watakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya ufunguzi na wataondoka madarakani baada ya muda huo lakini wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

(b) kama Bodi au mjumbe yeyote wa kamati ya afya anataka kujiuzulu, mjumbe huyo ataweka katika maandishi lengo lake kwa kipindi cha mwezi mmoja kwa katibu wa Bodi ya kamati ya afya.

Tangazo la Serikali Na. 161 (linaendelea)

(c) Endapo nafasi yoyote ya mjumbe wa Bodi itaachwa wazi kwa sababu ya kifo, kujiuzulu au ulemavu utakaomfanya ashindwe kushiriki kikamilifu kama mjumbe au kwa sabau nyingine yoyote ile, mjumbe mwingine atateuliwa kuziba nafsi hiyo na Halmashauri ndani ya kipindi cha miezi mitatu, kufuatia mapendekezo kutoka kamati ya maendeleo ya kata (WDC) na kupitishwa na timu ya wataalam wa Halmashauri, ikizingatiwa kwamba mjumbe huyo atakuwa madarakani kwa kipindi kilichobaki cha yule ambaye nafasi yake imechukuliwa.

(d) Mjumbe aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha 3 hapo juu anaweza kuchaguliwa katika uchaguzi mwingine.

(e) Pale ambapo Bodi au kamati nyingine yoyote iliyoanzishwa na Hati hii inakufa, wajumbe wote wa Bodi au kamati iliyokufa watasitisha uanachama na watapoteza nafasi zao.

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi imebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio la kikao cha Halmashauri kilichokaa tarehe 11 mwezi Desemba mwaka 2012 mbele ya:-.

ERICA MUSSIKA,
Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji
Bariadi

L.S.

ROBERT LWEYO MGATA,
Mwenyekiti
Halmashauri ya Mji
Bariadi

NAKUBALI,

Dodoma,
15 Machi, 2013.

MHE. MIZENGO P. PINDA (MB.),
Waziri Mkuu

TANGAZO LA SERIKALI NA. 162 la tarehe 07/06/2013

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 288)

———

SHERIA NDOGO

———

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)

———

SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI ZA MWAKA 2013.

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Mji wa Bariadi za mwaka 2013 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye *Gazeti* la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo:-

"ada ya mtumiaji" maana yake ni kiasi cha fedha anayolipa mtumiaji huduma kwa hospitali, kituo cha afya au zahanati, kwa ajili ya huduma ya afya itakayotolewa kwa mtumiaji;

"Asasi" maana yake ni pamoja na shule, vyuo, vikundi mbalimbali vilivyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria au asasi yoyote itakayokuwa imekubaliwa na kuidhinishwa na Bodi;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri iliyoundwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji); Sura 288

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Bariadi;

"huduma za afya" maana yake ni huduma zote za afya zinazotolewa na hospitali za Serikali na watu binafsi, na zinajumuisha huduma nyingine za afya zilizoanzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za afya ikiwa ni pamoja na vituo vya afya na Zahanati;

"kadi" maana yake ni kadi itakayotolewa na Bodi kwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

"kaya" maana yake ni:-

(a) mama, baba, watoto wenye umri chini ya miaka kumi na nane;

(b) mwanachama yeyote aliyefikisha umri wa miaka kumi na nane au zaidi na awe na mtoto au bila mtoto mwenye umri wa miaka kumi na nane;

(c) Taasisi au asasi yoyote.

"kituo cha huduma kilichoteuliwa" maana yake ni kituo kinachotoa huduma za afya na ni pamoja na kituo chochote kilichoanzishwa au kinachoendeshwa kwa malengo ya kutoa huduma za afya kiwe kinamilikiwa na Halmashauri, Serikali, asasi ya kidini, mtu au watu binafsi ambacho kinahusika na mfuko wa Afya ya Jamii;

"malipo ya huduma" maana yake ni malipo yanayotozwa na kituo cha tiba, kilichoteuliwa kwa watu ambao sio wanachama, wanapopatiwa huduma za afya katika kituo hicho;

"mchango au ada ya mwanachama" maana yake ni mchango wa hiari utakaotolewa na wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

"Mfuko au Mfuko wa Afya ya Jamii"(CHF) maana yake ni mfuko wa afya ya jamii wa tiba kwa kadi ulioanzishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

"Mganga Mkuu" maana yake ni Daktari ambaye ni msimamizi mkuu wa shughuli za huduma za afya katika Halmashauri;

"Mratibu" maana yake ni mratibu wa mfuko wa afya ya jamii;

"mwanachama" maana yake ni kaya inayochangia kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii;

"tele kwa tele" maana yake ni jazilio la asilimia mia moja fedha ambazo Halmashauri itapokea kutoka serikalini inayolingana na makusanyo ya michango ya wanachama wa mfuko wa afya ya jamii;

"Waziri" maana yake ni Wizara yenye dhamana ya masuala ya afya.

Mfuko wa Afya ya Jamii wa Tiba kwa Kadi

4.–(1) Kutakuwa na Mfuko wa Afya wa Jamii ambao ni mfuko wa hiari wenye lengo la kutoa huduma za afya, ambapo kaya zitakuwa zikilipia huduma hizo na Serikali itatoa mchango wake wa fedha kama jazilio kwa michango kutoka kwenye kaya; (tele kwa tele).

(2) Matumizi ya fedha yatafanywa na kusimamiwa na Bodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Madhumuni ya Mfuko

5. Madhumuni ya Mfuko yatakuwa ni:-

(a) kutafuta vyanzo vya fedha kutoka katika jamii kwa ajili ya kutoa huduma bora za afya kwa wanachama;

(b) kutoa huduma bora za afya zinazopatikana kwa kutumia mipango endelevu ; na

(c) kuboresha huduma za afya katika jamii kwa kugawanya madaraka na kuzipa nguvu jamii katika kufanya matumizi na kuchangia katika masuala yanayohusu afya zao.

Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii

6.–(1) Kutakuwa na Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi baada ya kupokea mapendekezo kutoka Timu ya Wataalam wa Afya wa Halmashauri (CHMT).

(2) Majukumu ya Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii yatakuwa kama ifuatavyo-

(a) kufuatilia, kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii kwenye vituo vya kutolea Huduma za Afya ya Jamii kwa kiwango kati ya Halmashauri, Jamii na wadau mbalimbali kwa ushirikiano na mhasibu wa Mfuko; na

(b) kuandaa taarifa za Mfuko wa Afya ya Jamii za robo mwaka na mwaka kwa kushirikiana na mhasibu wa Mfuko, pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na Halmashauri.

Muundo wa Bodi

7.–(1) Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao-

(a) wawakilishi wanne wa watumiaji huduma za afya kati yao wawili ni lazima wawe ni wanawake;

(b) mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za Afya binafsi bila faida na;

(c) mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za Afya kwa faida waliochaguliwa na Halmashauri kutoka vituo vya kutolea huduma za afya binafsi kwa faida waliochaguliwa miongoni mwao;

(d) mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji;

(e) Afisa Mipango wa Halmashauri;

(f) Mganga Mkuu wa Halmashauri ambaye atakuwa Katibu wa Bodi;

(g) mwakilishi mmoja kutoka Hospitali ya Halmashauri; na

(h) Mwakilishi mmoja kutoka Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa.

(2) Mwenyekiti wa Bodi atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe waliotajwa katika aya (a) - (c) ya kifungu kidogo cha (1).

(3) Ukiacha Wajumbe waliotajwa katika aya (a) - (d), Wajumbe waliotajwa katika aya (e) - (h) za kifungu kidogo cha (1) hawatakuwa na haki ya kupiga kura katika maamuzi ya Bodi.

Kazi za Bodi

8.–(1) Ili kufanikisha malengo yake makuu, Bodi itakuwa na kazi zifuatazo-

(a) itasimamia masuala na shughuli zote zinazohusu Mfuko wa Afya ya Jamii;

(b) itafanya kazi kwa kushauriana na Timu ya Uendeshaji ya Huduma za Afya ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa huduma ya afya inayotolewa ni bora na ya kitaalamu;

(c) kukusanya na kusimamia mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii;

(d) Kupokea, kuhakiki na kupendekeza kwa Halmashauri watu wanaostahili kusamehewa kutoa mchango kwenye Mfuko;

(e) kuweka malengo ya Mfuko;

(f) kupitia ripoti na taarifa kutoka Kamati ya Afya ya Kata au chanzo kingine chochote;

(g) kuratibu makusanyo, matumizi na kudhibiti mapato na;

(h) kupanga mipango ya afya ya mwaka kwa ajili ya kuthibitishwa na Halmashauri;

(i) kupanua na kuongeza utoaji wa huduma za afya kwa wanachama kulingana na mapato ya mfuko.

(2) Bodi katika kutekeleza majukumu yake, itapokea na kutekeleza maagizo ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria, kanuni na taratibu.

Sifa za wajumbe wa bodi

9. Mjumbe wa Bodi atakuwa na sifa zifuatazo-

(a) awe Raia wa Tanzania isipokuwa kwa wawakilishi kutoka katika Taasisi zisizo za kiserikali;

(b) awe na umri si chini ya miaka ishirini na tano na si zaidi ya miaka sabini;

(c) awe amehitimu elimu ya sekondari na kuendelea;

(d) awe na uzoefu na amewahi kuonyesha uwezo wake wa kuongoza katika shughuli za huduma jamii;

(e) awe na sifa ya uongozi;

(f) asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa; na

(g) awe mwanachama hai wa Mfuko wa Afya ya Jamii au Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Muda wa kukaa madara-kani

10.–(1) Mjumbe wa Bodi atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe aliyochaguliwa na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha miaka mitatu tu.

(2) Endapo nafasi yoyote ya mjumbe wa Bodi itaachwa wazi kwa sababu ya kifo, kujiuzulu, kukiuka maadili ya kazi au ulemavu utakaomfanya ashindwe kushiriki kikamilifu kama mjumbe au kwa sababu nyingine yoyote ile, mjumbe mwingine atachaguliwa kujaza nafasi hiyo iliyoachwa wazi.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2), haitaruhusiwa kuchagua mjumbe mwingine iwapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita.

Mikutano ya Bodi

11.–(1) Mikutano ya kawaida ya Bodi itaitishwa na Mwenyekiti kila robo mwaka.

(2) Ikiwa kuna umuhimu, Mwenyekiti anaweza akaitisha kikao cha dharura kulingana na mahitaji maalumu.

Uwajibikaji wa Bodi

12. Bodi itawajibika kwa Halmashauri kupitia Kamati husika.

Vyanzo vya Mapato

13. Vyanzo vya mapato ya Mfuko vitatokana na-

(a) fedha zote zitakazopokelewa kutokana na michango ya wanachama;

(b) ruzuku kutoka kwenye Halmashauri, Serikali Kuu, na wahisani mbalimbali toka ndani na nje ya Halmashauri;

(c) michango ya watu binafsi wanaoishi ndani na nje ya Halmashauri;

(d) malipo ya fedha ya wasiokuwa wanachama wa Mfuko kwa kupata huduma ya afya;

(e) ushuru utakaotozwa na Halmashauri kutoka vyanzo mbalimbali na kutengwa kwa ajili ya Mfuko; na

(f) fedha zozote halali ambazo Mfuko unaweza kupata toka mahali pengine popote;

(g) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; na

(h) fedha zozote halali ambazo Mfuko unaweza kupata kutoka mahali pengine popote.

Akaunti ya mfuko wa Bodi na watiaji saini

14.–(1) Kutakuwa na akaunti maalumu itakayotumika na Halmashauri ambayo fedha zote zitakazokusanywa kwa ajili ya Mfuko zitahifadhiwa na kutolewa.

(2) Malipo yataidhinishwa na Mkurugenzi kwa kufuata taratibu za kanuni za fedha za Halmashauri.

(3) Watia saini wa akaunti ya Mfuko watachaguliwa na Bodi na watakuwa ni mmoja kutoka kaundi “A” na “B” na kwa namna yoyote hakuna pesa zitakazotolewa kwenye akaunti ya mfuko bila saini ya mmojawapo kutoka kundi “A” na “B”.

(4) Watia saini kwenye hundi za Mfuko watakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Mwenyekiti wa Bodi na mjumbe mmoja wa Bodi ambao watakuwa Kundi "A";

(b) Katibu wa Bodi (Mganga Mkuu) na Mweka Hazina wa Halmashauri watakuwa Kundi "B".

(5) Kila baada ya miezi mitatu, Bodi itakuwa inatoa taarifa ya akaunti ya Mfuko kwa Halmashauri.

(6) Akaunti ya Mfuko itakaguliwa na wakaguzi waliochaguliwa kwa mujibu wa kanuni za fedha za Serikali za Mitaa.

Taarifa ya fedha ya mwaka

15. Mwezi mmoja baada ya mwaka wa fedha wa Halmashauri, bodi itatakiwa kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha ya mwaka na kuwasilisha kwa Halmashauri.

Mipango na Matumizi

16.–(1) Miezi miwili kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha wa Halmashauri, Bodi itaandaa mipango na bajeti ya mwaka kwa kuonyesha kiwango kinachotarajiwa kupatikana na mgawanyo wa fedha kwa ajili ya utoaji huduma za afya na maendeleo katika maeneo ya Halmashauri.

(2) Bodi inaweza kuandaa bajeti ya nyongeza kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo na kama mazingira yataruhusu.

(3) Mipango ya bajeti ya Mfuko itaandaliwa kulingana na utaratibu kama ilivyoainishwa katika vifungu vidogo vya (1) na (2) hapo juu, ambayo ni lazima iwasilishwe kwa Halmashauri kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

(4) Matumizi yatazingatia mipango shirikishi ya maeneo husika ambayo itakuwa sehemu ya Mpango kabambe wa afya wa Halmashauri. Mipango hii pia itazingatia maelezo yaliyomo ndani ya Mkataba wa tele kwa tele.

Usimamizi wa Mfuko

17. Usimamizi na uendeshaji wa Mfuko utakuwa chini ya:-

(a) Halmashauri kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri katika ngazi ya Halmashauri; na

(b) Kamati ya Maendeleo ya Kata kupitia Kamati ya afya ya Kata, katika ngazi ya Kata.

Kamati ya Afya ya kata

18. Kutakuwa na Kamati ya Afya ya Kata.

Wajumbe wa Kamati ya Afya ya Kata

19.–(1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na wajumbe wafuatao-

(a) Diwani anayewakilisha Kata husika;

(b) Afisa Mtendaji wa Kata;

(c) Mwalimu Mkuu mmoja kutoka shule ya msingi na mmoja kutoka shule ya Sekondari ambayo ipo kwenye Kata husika;

(d) wajumbe wawili wanawakilisha jamii husika ambapo mmoja wao ni lazima awe mwanamke;

(e) Mganga au Mganga Msaidizi wa Kituo cha Afya, ambaye atakuwa Katibu wa Kamati;

(f) mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutokana na watu waliopendekezwa na Serikali za Mitaa zilizomo ndani ya eneo la Kata; na

(g) mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutoka kwenye vyama vya kijamii kutoka kwenye Kata.

(2) Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ya Kata atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe.

(3) Endapo Kamati ya Afya ya Kata itashindwa kutekeleza kazi zake, Halmashauri itatoa onyo au kuivunja na kufanya utaratibu wa uchaguzi wa wajumbe wengine katika muda usiozidi miezi mitatu.

Kazi na Majukumu ya Kamati ya Afya ya Kata

20.–(1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na majukumu yafuatayo-

(a) kuwahamasisha na kuandaa jamii kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii;

(b) kuandaa orodha na kuratibu idadi ya wajumbe wa Mfuko wa Jamii;

(c) kusimamia ukusanyaji wa michango ya Mfuko;

(d) kuratibu viwango vya uchangiaji kwenye huduma na afya;

(e) kupitia utendaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii na kutoa mapendekezo ya ufumbuzi;

(f) kuanzisha na kuratibu mipango ya Afya ya Jamii; na

(g) kuendesha mikutano ya wajumbe wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

(2) Kamati ya Afya ya Kata, itakaa kila baada ya miezi mitatu, na Katibu atatoa taarifa ya maandishi wiki moja kabla ya siku ya Kikao.

(3) Baada ya kikao Katibu atawasilisha muhtasari wa kikao hicho kwa Katibu wa Mfuko wa Wilaya.

Matumizi ya fedha za Mfuko

21. Fedha zitakazokusanywa na Mfuko zitatumika kwa madhumuni yafuatayo-

(a) masuala yanayohusiana na afya yaliyotajwa katika mpango wa afya na kuidhinishiwa na Wizara; na

(b) suala au shughulu yoyote muhimu ya afya kama itakavyoonekana inafaa na kama itaidhinishwa na Bodi.

Utoaji wa Kadi kwa wana-chama

22.–(1) Kila mwanachama wa Mfuko na wategemezi wake, atapewa Kadi baada ya kulipa mchango wake wa mwaka kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 24(1) cha Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa kuzingatia kanuni za mfuko wa afya ya jamii za mwaka 2004, kila mwanachama atakayepewa msamaha ni lazima atapewa kadi ya uanachama na Halmashauri itaweka utaratibu wa kulipia kadi hiyo.

Haki zza mwana-chama na Utoaji wa Huduma za afya

23. Kila mwanachama na wategemezi wake watakuwa na haki zifuatazo-

(a) kupata huduma ya afya aliyolipia anapougua ndani ya eneo la Halmashauri husika au katika kituo cha Afya kwenye Halmashauri nyingine ambayo itaingia makubaliano maalum na Halmashauri husika;

(b) kupata huduma ya afya kwa baba, mama na watoto wao wenye umri chini ya miaka kumi na nane;

(c) kutoa mapendekezo kuhusu huduma za afya kupitia kituo chake cha tiba ambayo yatafanyiwa kazi na Bodi; na

(d) kushirikishwa kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa huduma za afya, katika eneo la Halmashauri.

Kiwango cha mchango au ada ya mwana-chama

24.–(1) (a) Mtu yoyote atakayetaka kuwa mwanachama wa mfuko wa afya ya jamii atapaswa kutoa mchango au ada ya uanachama ya kiasi cha shilingi elfu kumi (10,000) kila mwaka;

(b) mchango huo utalipwa na kila mtu anayetaka kuwa mwanachama wa mfuko mwanzoni mwa mwaka au kila mwaka wa fedha unapoanza au kama Bodi itakavyoelekeza;

(c) mtu yoyote ana hiari ya kulipa mchango wake wa uanachama kwa zaidi ya mwaka mmoja.

(2) Bila kuathiri kifungu cha 21(c) hapo juu mtu yeyote anayelipa mchango wa uanachama kwa zaidi ya mwaka mmoja, pale inapotokea mabadiliko ya kiwango cha mchango atawajibika kulipa tofauti ya kiwango kilichozidi kile cha awali.

(3) Halmashauri itaandaa utaratibu wa kupanga kaya maalum zilizoko katika Taasisi/shule mbalimbali zilizo ndani ya Halmashauri ili kuziwezesha kupata huduma.

Muda wa uana-chama

25.–(1) Mtu yoyote atabaki kuwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii kila atakapolipa ada yake ya mwaka.

(2) Kila mwaka unapoisha uanachama wa mtu utafikia mwisho hadi pale atakapotimiza msharti ya kifungu kidogo cha (1).

Malipo ya papo kwa papo

26.–(1) Mtu yoyote ambaye hatakuwa mwanachama wa mfuko huu, atalipa mchango au malipo ya papo kwa kila atakapoenda kupata matibabu katika kituo cha kutolea huduma za Afya.

(2) Malipo ya papo kwa papo yatalipwa kama ifuatavyo-

(a) shilingi elfu moja (1,000/=) katika huduma za afya zinazotolewa na Zahanati katika eneo lolote la Halmashauri;

(b) shilingi elfu moja mia tano (1,500/=) kwa huduma za Afya zinazotolewa na kituo cha Afya kilichopo ndani ya Halmashauri;

(c) huduma za Hospitali za aina zote kulingana na Sera ya uchangiaji.

Misamaha kwa wasio-jiweza

27. Misamaha kwa wasioweza kulipa gharama za matibabu itatolewa na kulipwa na Halmashauri baada ya kuzingatia utaratibu ufuatao:-

(a) Serikali ya Mtaa katika vikao vyake itapokea, itajadili na kuwasilisha orodha sahihi kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata;

(b) Kamati ya Maendeleo ya Kata itapokea, itajadili na kuwasilisha orodha sahihi ya wasioweza kulipa gharama za matibabu kwa Bodi ya Afya ya Halmashauri; na

(c) Bodi ya Afya itapokea, na kujadili mapendekezo husika na kuyawasilisha pamoja na gharama zake kwa Halmashauri kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

Makosa

28. Mtu yeyote ambaye-

(a) atakwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi;

(b) atafanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi kufanya kazi zake kwa ufanisi;

(c) atatumia vibaya mali na rasilimali za Mfuko na kusababisha kutofikia malengo ya Bodi;

(d) atatumia vibaya madaraka aliyonayo kumzuia afisa wa Bodi kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii; au

(e) atashindwa kwa uzembe kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) na isiyozidi shilingi laki tatu

300,000/=) au kwenda jela kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi imewekwa kufuatia azimio la Baraza la Mji la tarehe 11 mwezi Desemba mwaka 2012 mbeya ya:

.....
ERICA MUSSIKA,
Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji Bariadi

L.S

.....
MHE. ROBERTH LWEYO MGATA,
Mwenyekiti
Halmashauri ya Mji Bariadi

NAKUBALI,

.....
MHE. MIZENGO PETER PINDA (MB.),
15 Machi, 2013 *Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 163 la tarehe 07/06/2013

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 288)

———

SHERIA NDOGO

———

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)

———

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI ZA MWAKA 2013

Jina na mwanzi wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Mji wa Bariadi, 2013 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo:-

"Afisa Muidhinishwa" maana yake ni Afisa Maliasili, Afisa Kilimo na Mifugo na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"eneo la Hifadhi" ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Bariadi;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Muidhiniwa chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote;

"kiwanda" maana yake ni jengo au kundi la majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa;

"kuvuna misitu" maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au kung'oa miti, visiki;

"maeneo ya malisho" maana yake ni pamoja na sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri;

"maji" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi Mazingira ni pamoja na maji ya kunywa, ya mito, vijito, maji yanayotiririka, yanayohifadhiwa, yaliyo katika visima, mabwawa, mifereji, madimbwi, maziwa, maji yaliyoko chini ya ardhi na maji yaliyoko katika mkondo; Sheria Na. 20 ya mwaka 2004

"maji taka" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi, majengo ya biashara na viwanda; Sheria Na. 20 ya mwaka 2004

"mazao ya misitu" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu chini ya kifungu cha 2 ni kitu chochote kinachopatikana au kuzalishwa kutokana na miti, mazao yanayoota au kupatikana msituni, ambayo ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao, mbegu za miti, nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani, mizizi, gundi, utomvu, maranda matete, kamba, makuti mawale, nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu chochote chenye uhai au kisicho na uhai kitakachotangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa ni zao la misitu; Sheria Na. 14 ya mwaka 2002

Sheria Na. 20 ya mwaka 2004

"mazingira" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira yanahusisha maumbile halisi ya wazungukao Binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia ya nchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, viumbe hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa binadamu na jinsi yanavyoingiliana;

"mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mifugo" maana yake ni mnyama yeyote anayefugwa na binadamu;

"misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asilia au liyopandwa, au asilimia 50 au zaidi, ya vichaka na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya sheria ya misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

Sheria Na. 14 ya mwaka 2002

Sheria Na. 20 ya mwaka 2004

"taka" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira maana yake ni kitu chochote kimiminika, kugumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira;

Sheria Na. 20 ya mwaka 2004

"taka ngumu" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani. Katika majengo ya biashara, viwanda na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi, pastic au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo, utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps);

"taka za viwandani" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, maana yake ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa au mawasiliano, pamoja na taka nyingine ngumu kama zilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira Sehemu IX;

Sheria Na. 20 ya mwaka 2004

"uchafu hatari" kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004. Maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji. gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia, kwa binadamu, au mazingira;

"Uchafuzi wa Mazingira" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ni mabadiliko ya hali ya hewa ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja, joto, kemikali, biolojia, au zana za mionzi katika mazingira ambayo zana hizo zinafanyia kazi au kutoa harufu mbaya, mrundikano wa taka ambazo unaathiri watumiaji, au unaosababisha hali hatari kwa afya ya jamii, usalama, au ustawi, au hatari kwa wanyama, ndege, wanyama pori, samaki, au viumbe vyote vya baharini, mimea au kusababisha hali mbaya ya hewa, upungufu au kizuizi ambacho ni sehemu katika Sheria Ndogo hizi; Sheria Na. 20 ya mwaka 2004

"udongo" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira maana yake ni pamoja na mchanga, miamba, tope, madini, uoto wa mimea, mimea na wanyama iliyoko chini ya udongo pamoja na vumbi; Sheria Na. 20 ya mwaka 2004

"vitu hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ni kemikali yoyote, taka, gesi, madawa, vidonge, mimea, wanyama au viumbe hai visivyoonekana ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu, maisha au mazingira; Sheria Na. 20 ya mwaka 2004

"Waziri" maana yake ni waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

SEHEMU YA PILI
MASHARTI YA UFUGAJI

Wajibu wa mfugaji

4.–(1) Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi-

(a) atatakiwa kufuga idadi ya mifugo kama itakavyoainishwa katika kibali chake kitakachomruhusu kufuga kwa kuzingatia ukubwa wa eneo la kuridhika kwamba ufugaji huo hautakuwa kero kwa majirani;

(b) atatakiwa kufuga ndani ya eneo lake (zero grazing) bila ya kuleta usumbufu kwa jirani zake na jamii kwa ujumla na kuhakikisha sehemu ya kufugia wanyama hao inakuwa safi wakati wote na ana chombo cha kuhifadhi samadi inayotokana na mifugo hiyo;

(c) anayeishi pembezoni mwa Mji atatakiwa kupitisha mifugo yao katika njia zilizopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri;

(d) atatakiwa kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;

(e) atatakiwa kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa kufanya hivyo;

(f) atatakiwa kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamuriwa na Halmashauri na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo.

Masharti ya mfugaji

5. Ni marufuku kwa mfugaji yeyote-

(a) kuchunga, kulisha na kunywesha maji mifugo katika maeneo ya mipango miji pamoja na maeneo yote ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo;

(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;

(c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi jingine bila kubali kutoka kwa Halmashauri;

(d) kuuza au kununua mifugo katika meeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri;

(e) kufuga mifugo mingi katika eneo dogo la Halmashauri;

(f) kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayakuodhinishwa na Halmashauri kupitisha mifugo.

Kudhibiti mifugo inayo-zurura ovyo

6.–(1) Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wowote utakaoonekana unazurura hovyo katika eneo la Halmashauri ambapo hapajaruhusiwa kuchungia mifugo.

(2) Mfugo wowote utakaokamatwa utaliiwa faini kama ilivyooneshwa kwenye jedwali na baada ya kulipia gharama hizo mfugaji atarudishiwa mifugo yake.

(3) Endapo mwenye mifugo au mfugo hatatokea ndani ya siku saba (7) tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo au mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Baada ya mauzo, Mkurugenzi atakata fedha za faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mifugo na kama hataonekana ndani ya siku kumi na nne (14) fedha hizo zitaingizwa katika vyanzo vya mapato ya Halmashauri.

(5) Endapo mwenye mifugo hiyo atakuwa na sababu za msingi za kutofika kwake katika muda wa siku kumi na nne (14) Halmashauri itarudisha fedha zake.

(6) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo au mfugo Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote.

Ukaguzi wa mifugo

7.–(1) Itakuwa halali kwa Afisa Kilimo na Mifugo, Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji, na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi kuingia katika nyumba au jengo lolote wakati wowote kwa madhumuni ya kukagua na kuhesabu idadi ya mifugo iliyomo katika nyumba hiyo.

(2) Mtu yeyote atakayemzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa Halmashauri

Sheria Na. 20 ya mwaka 2004

8.–(1) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za malisho kwa kuzingatia idadi ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Sura ya 113 na 114 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

(2) Halmashauri itatenga njia maalum ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi malishoni au minadani.

(3) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi ya mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

Taratibu za ufugaji

9.–(1) Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyo katika Sheria Ndogo hizi au Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mfugo au mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinjia nyama mahali pengine popote.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kununua, kuuza au kufanya biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada ya magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo.

SEHEMU YA TATU
KILIMO NA HIFADHI YA ARDHI

Taratibu za kilimo

10.–(1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia sheria ya Ardhi Sura ya 113 na 114 na Sheria nyingine zitakazotungwa na Bunge.

(2) Itakuwa halali kwa Afisa Kilimo kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Masharti kwa mkulima

11.–(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulina katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakaloharibu hifadhi ya mazingira bila kuzingatia ushauri wa Afisa Kilimo Michango ya Jamii.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia kinyume ardhi iliyotengwa kwa matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalum kutoka kwa Halmashauri.

(4) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, terehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(5) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi.

(6) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia kilimo cha kuhamahama na kuhimiza kilimo cha mzunguko (crops rotation).

Uhifadhi wa uoto wa asili

12. Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake.

Uchimbaji mchanga na kokoto

13. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba mchanga katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa kando kando ya barabara, mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa katikati ya barabara.

14. Ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga nyumba au jengo lolote katika eneo la hifadhi.

SEHEMU YA NNE
HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

15.–(1) Halmashauri itawajibika kuanzisha, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Maeneo yaliyotajwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi yamehifadhiwa.

(3) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

Kulinda eneo la hifadhi

16.–(1) Ni marufuku wa mtu yeyote kulima, kukata miti, kufuga mifugo katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha maji isipokuwa kwa ruhusa ya Halmashauri.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

17.–(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote, kiwanda, taasisi, shirika kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chmichemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vilivyo hai.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai.

SEHEMU YA TANO
HIFADHI YA MISITU

Kuchoma au kusababisha moto

18.–(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma misitu kwa namna yoyote ile katika misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(2) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka kuamuru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Kibali cha kuchoma moto

19. Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma moto atalazimika kutoa taarifa ya siku saba (7) kabla ya kuchoma moto kwa majirani walioko katika eneo analotaka kuchoma au ataweka njia za kuzuia moto.

Ukataji miti

20.–(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri.

(2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Ni marufuku wa mtu yeyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalum ambao ni rasilimali kwa Taifa.

(4) Watu wanao vuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Wajibu wa kupanda miti

21. Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika:-

(a) kupanda na kutunza miti katika eneo lake;

(b) kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki;

22. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila kijiji-

(a) kitawajibika kutenga eneo la hifadhi ya misitu wa asili kwa ajili ya matumizi ya baadae;

(b) kitalazimika kutunza miti yote inayopandwa katika eneo la kijiji;

(c) kitahakikisha ya kuwa kila kaya inapanda miti isiyopungua kumi kwenye eneo la nyumba yake;

(d) mtu yeyote anayetaka kukata miti au mti wa matumizi ya kuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi na shughuli nyinginezo, inabidi apate kibali cha maandishi toka kwa mwenyekiti wa kijiji, mtendaji wa kijiji na kibali cha Afisa Maliasili wa wilaya au wasaidizi wake kwa miti uliyopandwa na kuhifadhiwa na Halmashauri ya wilaya;

(e) kinapaswa kutenga na kupanda shamba la miti ekari 2 kila mwaka na kulitunza;

(f) kila shule au taasisi nyingineyo katika Halmashauri itapaswa kupanda miti ya kukinga upepo kuzunguka majengo yake;

(g) mitaa, kijiji kitapaswa kutunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye milima, makorongo na vyanzo vya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo;

(h) kijiji kitahakikisha kuwa kila anayeandaa shamba kwa ajili ya kilimo hatumii moto na anapanda miti kwenye mipaka ya shamba lake kama kinga upepo;

(i) kila mtu mwenye nyumba kwenye eneo la kati ya Mji atawajibika kupanda miti kando ya barabara inayopita mbele ya nyumba yake na kuitunza;

(j) kila Mwenyekiti wa Mtaa, Mtendaji wa kijiji, mkuu wa taasisi yoyote atahakikisha kuwa ina msitu wa hifadhi wa miti ya kupandwa au ya asili uliyotengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi ardhi, mazingira na matumizi ya baadaye.

SEHEMU YA SITA
HIFADHI (MAKABURI)

23.–(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga maeneo ya makaburi na kuhakikisha maeneo hayo yanakuwa katika hali ya usafi na usalama.

(2) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuzika mwili wa binadamu katika maeneo ambayo hayakutengwa na Halmashauri ya Mji au vijiji.

(3) Iwapo mtu yeyote atataka kuzika eneo tofauti na lililotengwa atapaswa kuomba kibali kutoka Halmashauri ya Mji.

SEHEMU YA SABA
TAKA NGUMU NA LAINI

24.–(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake.

(2) Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini, au kujisaidia/kuoga katika kingo za maziwa, mabwawa, mito au kwenye vyanz vya maji vilivyoko katika Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Undeshaji wa viwanda

25. Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

SEHEMU YA NANE
MAKOSA NA ADHABU

Makosa yanayohusu mifugo

26. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa:

(a) ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(b) atasafirisha mifugo bila kuwa na kibali;

(c) atalisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;

(d) atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa;

(e) atavua samaki kwa kutumia sumu au nyavu zenye matundu madugo (kokoro).

Makosa yanayohusu kilimo

27. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchanga, kokoto, madini katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu kuhifadhi ardhi

28. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kuhifadhi ardhi atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu vyanzo vya maji

29.–(1) Mtu yeyote atakayeharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji atakuwa ametenda kosa.

(2) Mtu yeyote atakayebainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine ambao ni rasilimali ya Taifa atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu kuharibu misitu

30. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa:

(a) atachoma au kusababisha moto katika msitu bila kibali, au

(b) atashindwa kushiriki katika kuzima moto;

(c) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa isiyohifadhiwa bila kibali;

(d) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali; au

(e) atafyaka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye eneo bila kibali;

(f) atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa miti iliyohifadhiwa kama bustani ya miti;

(g) atakata miti, au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kinga upepo;

(h) atabandua magome ya miti kwa ajili ya kutengeneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila ya kuwa na kibali; au

(i) atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

Makosa yanayohusu taka ngumu na laini

31. Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini katika eneo lolote lisiloruhusiwa atakuwa ametenda kosa kutokana na Sheria Ndogo hizi au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

32. Mtu yeyote atakayetiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu viwanda

33. Mtu yeyote atakayeendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa nafaka mashine za kuranda katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji atakuwa ametenda kosa.

34. Mtu yeyote atakayevunja masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini kama inavyooneshwa kwenye Jedwali.

adhabu

35. Mtu yeyote atakayevunja masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini kama inavyooneshwa kwenye Jedwali.

JEDWALI
(Chini ya kifungu cha 33 na 34)

NA.	KOSA	KIFUNGU	ADHABU
1.	Mifugo kuzurura ovyo	6(2)	Faini ya shilingi 5,000 kwa kila ng'ombe 3,000 kwa kila mbuzi/kondoo
2.	Kulisha na kunywesha mifugo sehemu zisizoruhusiwa	5(a)	Faini ya shilingi 5,000 kwa kila ng'ombe 3,000 kwa kila mbuzi/kondoo
3.	Kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani	5(b)	Faini ya shilingi 5,000 kwa kila ng'ombe 3,000 kwa kila mbuzi/kondoo
4.	Kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali kusafirisha mifugo bila kibali	5(d) 5(c)	Faini ya shilingi 5,000 kwa kila ng'ombe 3,000 kwa kila mbuzi/kondoo Faini ya shilingi 50,000/=
5.	Kuuza au kununua mifugo maeneo yasiyoruhusiwa	5(d)	Faini ya shilingi 50,000/=
6.	Kulisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa	5(a)	Faini ya shilingi 5,000 kwa kila ng'ombe 3,000 kwa kila mbuzi/kondoo

NA.	KOSA	KIFUNGU	ADHABU
	Kufuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa	4(a)	Faini ya shilingi 50,000/=
7.	Atakayewazuia maafisa kufanya kazi saa za kazi	7(2)	Faini ya shilingi 50,000/=
8.	Kuchinja mifugo nje ya eneo lililoruhusiwa au bila idhini ya afisa mifugo	9(2)	Faini ya shilingi 50,000/=
9.	Ukiukwaji ya masharti ya kilimo	10-14	Faini ya shilingi 50,000/=
10.	Uharibifu wa vyanzo vya maji na kushindwa kuhifadhi vyanzo hivyo	15(2)	Faini ya shilingi 100,000/=
11.	Kuweka sumu ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe hai	17(2)	Kama itakavyoamriwa na mahakama
12.	Kuchoma moto kwa ajili ya kusafisha shamba au kuchoma misitu bila kibali	11(3) & 18(1)	Faini ya shilingi 50,000/=
	Kushindwa kushiriki katika kuzima moto	18(2)	Faini ya shilingi 50,000/=
13.	Kuvuna mazao ya misitu iliyohifadhiwa bila kibali Kuchoma mkaa na kukata kuni bila kibali	29(c)	Faini ya shilingi 100,000/= na mali hiyo itaifishwe
14.	Kufyeka nyasi, kung'oa vichaka na visiki kwenye misitu iliyohifadhiwa bila kibali	29(e)	Faini ya shilingi 50,000/=
	Kuchunga mifugo kwenye eneo lililopandwa miti au lililohifadhiwa kama bustani	29(f)	Faini ya shilingi 50,000/=
	Kubandua magome ya miti bila ya kibali kulima na kukata miti katika vyanzo vya maji	29(h)	Faini ya shilingi 50,000/=
15.	Kutupa taka ngumu na laini ovyo	30	Faini ya shilingi 50,000/=

NA.	KOSA	KIFUNGU	ADHABU
	Kutiririsha maji machafu ovyo	31	Faini ya shilingi 50,000/=
16.	Uendeshaji wa shughuli za viwanda, karakana, mashine za kusaga, kukoboa na kukamua mashine za kuranda kuchomelea vyuma na shughuli yoyote inayozalisha uchafu kwenye makazi ya watu bila kufuata taratibu za mipango miji	32	Faini ya shilingi 100,000/=
17.	Makosa mengine ambayo yemeainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi		Faini ya shilingi 50,000/=

Muhuri ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 11 mwezi Desemba mwaka 2012 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

ERICA MUSSIKA,
Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji Bariadi

L.S

ROBERT LWEYO MGATA,
Mwenyekiti
Halmashauri Mji Bariadi

NAKUBALI,

MIZENGO PETER PINDA (MB.),
Waziri Mkuu

15 Machi, 2013

Tangazo la Serikali Na. 164 la Tarehe 7/6/2013

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(Sura ya. 290)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya Vifungu 6(3) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (KODI YA MAJENGO) ZA HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI ZA MWAKA 2013

Jina la mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kodi ya Majengo) za Halmashauri ya Mji wa Bariadi za Mwaka 2013 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa bariadi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Bariadi na eneo lake la kiutawala;

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni mtu au Afisa yeyote aliyeruhusiwa na Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza Sheria Ndogo hizi;

"mali" maana yake ni kiwanja, jengo, nyumba na inajumuisha uendeshaji wa nyumba au jengo kwa umbo lake;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi;

"Ushuru" maana yake ni ushuru wa mali unaotozwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"jengo" maana yake ni nyumba au jengo lolote linalotumika kwa ajili makazi ya mtu/watu au nyumba au jengo lolote linalotumika kwa shughuli za kibiashara tu pia inajumuisha nyumba inayotumika

kwa shughuli za makazi na biashara kwa pamoja;

"ghala" maana yake ni jengo au nyumba inayotumika kwa matumizi ya kuhifadhia vitu mbalimbali;

"kiwanda" maana yake ni jengo linalotumika kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa ukarabati au ukarafati wa vitu mbalimbali;

"ghorofa" maana yake ni jengo lenye ghorofa zaidi ya moja.

Usajili

4. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa jengo ndani ya eneo la Halmashauri, kuhakikisha kwamba jengo lake limesajiliwa na Halmashauri na kupewa namba maalum ya utambuzi ya mlipa Kodi ya Majengo na namba hiyo ibandikwe sehemu ya wazi inayoonekana.

Wajibu wa mmiliki

5. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki ambaye anamiliki jengo ndani ya Halmashauri:-

(a) kulipa kodi ya majengo kama ilivyoelekezwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi;

(b) kuhakikisha kuwa jengo lake limesajiliwa na kuingizwa kwenye orodha ya walipa kodi.

Muda wa kulipa kodi Msamaha wa kodi

6.-(1) Kodi ya Majengo itozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi italipwa kwa Halmashauri au Wakala wake kuanzia tarehe 1 Julai na mwisho wa malipo hayo itakuwa kila au kabla ya tarehe 30 ya mwezi wa machi ya kila mwaka.

(2) Baada ya tarehe iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) hapo juu, kila mmiliki wa mali ambaye atakuwa hajalipa ushuru huo, atalazimika kulipa ushuru pamoja na faini ya asilimia hamsini (25%) ya deni lote.

(3) Baada ya tarehe thelathini na moja ya mwezi Machi ya kila mwaka, endapo mtu huyo atashindwa kulipa kodi baada ya muda wa notisi ya siku kumi na nne (14) kupita, Halmashauri itaomba Mahakama yenye mamlaka amri ya kukamata au kushikilia mali ya mdaiwa kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

Uteuzi wa wakala

7. Halmashauri inaweza kupunguza au kufuta kabisa Kodi ya Jengo kwa majengo yaliyoorodheshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa wakala

8.-(1) Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kukusanya ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kukusanya kodi ya majengo atakuwa na wajibu wa:-

(a) kukusanya na kupokea Kodi kutoka kwa kila mmiliki ambaye anawajibika kulipa Kodi ya Majengo na kuwasilisha malipo hayo Halmashauri kwa tarehe na utaratibu utakaokuwa umeainishwa kwenye mkataba;

Makosa ya wakala

(b) kutoa taarifa kwa Halmashauri jina la mtu aliyeshindwa au kukataa kulipa Kodi.

(3) Wakala yeyote ambaye:-

(a)atashindwa kuwasilisha Halmashauri kiasi cha Kodi alichokusanya;

(b) kwa makusudi atadai kutoka kwa mmiliki yeyote kiasi cha fedha kuzidi alichotakiwa kutozwa;

(c) kwa makusudi atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri;

(d) atashindwa kutekeleza majukumu yake aliyopewa kama Mkusanya Kodi chini ya Sheria Ndogo hizi.

atakuwa ametenda kosa na atashitakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote faini na kifungo pamoja kulipa hasara atakayokuwa ameisababishia Halmashauri.

Makosa na adhabu

9. Mmiliki yeyote ambaye atakataa au kushindwa kulipa Kodi ya Majengo au kushindwa kusajili jengo atakuwa ametenda kosa na atashitakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atatuhumiwa kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo

kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo pamoja na hasara atakayokuwa ameisababishia Halmashauri.

Kufifilisha kosa

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu yeyote isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kutenda kosa hilo kwa kujaza fomu maalum iliyopo kwenye jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini anayodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

A

S/No	Aina ya Kiwanja/ Nyumba/Jengo	Matumizi ya mali	Kiasi
1.	Eneo dogo (Ujazo Mdogo)	i. Makazi ii. Biashara iii. Makazi ya biashara	5,000/= 10,000/= 15,000/=
2.	Eneo la kati (Ujazo wa Kati)	i. Makazi ii. Biashara iii. Makazi ya biashara	10,000/= 15,000/= 20,000/=
3.	Eneo kubwa (Ujazo Mkubwa)	i. Makazi ii. Biashara iii. Makazi na biashara	20,000/= 25,000/= 25,000/=
4.	Kiwanda	i. Matumizi ya viwanda	400,000/=
5.	Ghala	i. Biashara/ Makazi	200,000/=
6.	Nyumba kubwa	i. Biashara	50,000/=
7.	Nyumba kubwa	i. Biashara na Makazi	80,000/=
8.	Ghorofa	i. Biashara ii. Makazi	100,000/= 100,000/=

JEDWALI LA KWANZA

B

Taasisi	Kiasi	Muda
1. Benki	150,000/=	kwa mwaka
2. TTCL	50,000/=	kwa mwaka
3. Posta	50,000/=	kwa mwaka
4. Vituo vya mafuta	100,000/=	kwa mwaka
5. TANESCO	100,000/=	kwa mwaka
6. Nyumba za kulala wageni	30,000/=	kwa mwaka

JEDWALI LA PILI

FOMU YA SUMMARY WARRANT YA KUSHIKA NA KUUZA KWA DALALI WA MAHAKAMA

(Chini ya Kifungu cha 6(3) cha Sheria Ndogo hizi)

Hivi ni kukuamuru kukamata mali inayohamishika ya.....

kama ilivyooneshwa katika jedwali hapo juu atalipa kiasi cha shillingi..... ikiwa ni ushuru unaodaiwa na Halmashauri ya Mji pamoja na riba ya kiasi cha shilingi.....kwa kila mwezi au sehemu ya mwezi kutoka tarehe .....ya mwezi. .....mwaka .....

Na gharama za ukamataji huu na baada ya kumpatia kusudio la siku kumi na nne (14) na kuitarifu Mahakama muda huo na baada ya kufanya madai ya kuuza kwa mnada mali au sehemu ya mali itakayokidhi thamani ya shilingi.....kama ilivyofafanuliwa hapo juu.

Na unaamriwa tena kurudisha fomu hii siku au kabla ya siku ya.....

.....ya mwezi wa.....ya mwaka.....

ikiwa imesainiwa kuthibitisha jinsi ilivyotekelezwa au sababu za kutotekeleza.

Imetolewa kwa mkono wangu na mhuri wa Mahakama leo.....

.....siku ya mwezi.....wa mwaka.....

_____

JEDWALI LA TATU

_____

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

_____

(Chini ya Kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi)

Mimi.....*wa*

S.L.B.....ninaefanya biashara ya.....

katika eneo la.....lililopo ndani ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi. Nakiri kuwa leo tarehe.....Nilikiuka kifungu cha.....cha Sheria Ndogo za (Kodi ya Majengo) za Halmashauri ya Mji wa Bariadi za mwaka 2013. kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi.

Sahini.....

Mbele yangu.....(jina)

Saini.....

Wadhifa.....

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi imewekwa kufuatia Azimio la Halmashauri ya Mji la tarehe 11 mwezi Desemba mwaka 2012 mbele ya:

ERICA MUSSIKA,
Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji Bariadi

MHE. ROBERT LWEYO MGATA
Mwenyekiti
Halmashauri ya Mji Bariadi

NAKUBALI,

Dar es Salaam,
15 Machi, 2013

MIZENGO PETER PINDA,
Waziri Mkuu

Tangazo la Serikali Na. 165 la Tarehe 7/6/2013

SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(Sura. Na. 288)

(Zimetungwa chini ya Kifungu Na. 89

SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI ZA MWAKA 2013

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Mji wa Bariadi za mwaka 2013 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo-

"ada" maana yake ni kiwango cha fedha kilichowekwa na Halmashauri kulipia gharama za kuzoa taka kama zinavyooneshwa kwenye Jedwali lililoainishwa katika Sheria Ndogo hizi;

"Afisa Afya" maana yake ni Afisa yeyote anayesimamia kazi za afya na mazingira za Halmashauri;

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"bomba la maji" maana yake ni mtandao wa mabomba kwa ajili ya kusafirisha maji kutoka katika nyumba au sehemu nyingine ya maji taka yanapozalishwa;

"CBO" maana yake ni kikundi cha jamii kinachoundwa kwa ajili ya kutatua tatizo au kufanya shughuli ya maendeleo katika jamii ya eneo hilo ambapo CBO hiyo imeundwa;

"chombo cha takataka" ina maana ya pipa la taka lenye mfuniko au chombo kingine chochote kilichokubaliwa na Halmashauri ambacho kimewekwa na mwenye nyumba au mpangaji kwa ajili ya kuhifadhia takataka kutoka kwenye jengo husika;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinachotumika kama

chakula au kinywaji kwa binadamu isipokuwa vipodozi, dawa na inajumuisha:-

(a) kitu chochote kinachotumika kwa kutengeneza chakula;
(b) kitu chochote kinachowekwa kwenye chakula kama ladha;
(c) rangi yoyote inayowekwa kwenye chakula;

"chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho kimewekwa au kujengwa katika hali ya uchafu na kinaweza kusababisha:-
(a) madhara kwa maisha ya binadamu, wanyama au kiungo chake;
(b) cheye kuleta adha;
(c) kitu chochote kinachoweza kuhatarisha usalama, Afya na Mazingira ya Binadamu au wanyama;

"eneo lililozuiwa" maana yake ni maeneo yote ambayo majani marefu na mimea imepigwa marufuku kuwepo na inahusisha maeneo ya wazi, mitaa na barabara;

"halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Bariadi;

"huduma" maana yake ni kusafisha, kuondoa na kukusanya na kutupa taka za viwandani, biashara na za majumbani;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"kaya" maana yake ni makazi ya familia ya baba, mama, watoto na wategemezi wake au wao peke yao;

"kadi ya ukaguzi wa afya" maana yake ni kadi inayotolewa na wategemezi wake au wao peke yao;

"kadi ya ukaguzi wa afya" maana yake ni kadi inayotolewa na Halmashauri kila mwaka kuthibitisha uhalisi na usalama wa eneo la biashara pamoja na watoa huduma;

"kuzuia" maana yake ni kitendo kinachofanywa na mtu au kikundi cha watu kwa kukataza au kuashiria kukataza moja kwa moja Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi kwa kutumia nguvu au vitisho;

"magonjwa ya malipo" maana yake ni kipindupindu au magonjwa yanayofanana na hayo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"majani" maana yake ni majani au vichaka vyenye urefu wa sm 30 au zaidi na vingine vifananavyo na hivyo vilivyopo maeneo yaliyokatwazwa;

"maji taka" maji taka maana yake ni kinyesi au mkojo na uchafu

mwingine kama matapishi, mate na maji machafu yanayotokana na uoshaji nguo, maji ya kuoga na maji ya kupigia deki, kuosha vyombo, maji yanayotokana na mvua kwenye mitaa, pia uoshaji wa magari, maji yanayotokana na uchafu kutoka vituo vya mafuta na viwandani ambayo yana kemikali au asiyokuwa na kemikali na ambayo hayajasafishwa;

"makazi" maana yake ni nyumba, ghorofa au jengo lolote linalotumika kwa kuishi, pamoja na ardhi ambayo haijaendelezwa lakini imetolewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kuishi;

"mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania au raia wa kigeni ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko chini ya Mamlaka ya Halmashauri na ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"mtaa" maana yake ni sehemu ya mji iliyopo kwenye Halmashauri ya Mji kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

"mzigo wa taka" ni pamoja na pingili au sehemu za miti, matawi ya miti, vichaka vilivyofyekwa, magazeti, vijarada, masanduku ya karatasi au taka ngumu zilizofungwa kuwa mzigo uliofungwa vizuri au usiozidi mita moja kwa urefu au uzani wa kilo 15;

"mwenye nyumba" maana yake ni mtu yeyote anayemiliki nyumba kisheria, wakala wake au mpangaji;

"nyumba" maana yake ni jengo aina yoyote lililojengwa na linalojumuisha nyumba za makazi;

"premises" maana yake ni eneo la ardhi, majengo, magari, mabehewa ya treni au vyombo vingine vya kubebea, mahema, mikokoteni, gari la mizigo, chombo cha aina yoyote, mifereji, mkusanyiko wa maji unaofanya bwawa, ziwa, bahari, ufukwe, bomba la maji au eneo lolote lililo wazi au lililofunikwa likiwa limeendelezwa na bado kuendelezwa kisheria. pia inajumuisha vyombo vinavyoelea majini vikiwemo meli, mashua/mitumbwi, winchi au chombo chochote cha majini/ ziwa, mto, barabara au katika eneo lote lililo chini ya Halmashauri;

"rundo kubwa" maana yake ni zana kubwa, mashine, samani na taka ngumu nyingine isipokuwa marundo ya vitu vya ujenzi au mabaki ya majengo yaliyobomolewa, wanyama waliokufa wenye uzito mkubwa zaidi ya ule uliobainishwa kwenye mzigo wa taka (bundle waste);

"bomba la maji taka" maana yake ni mtandao wa mabomba kwa ajili ya kusafirisha maji taka kutoka katika nyumba au sehemu nyingine ya maji taka yanapozalishwa;

"soko" ina maana ya soko lililowekwa na Halmashauri kisheria au eneo ambalo linatambuliwa kisheria na Halmashauri ya Mji wa Bariadi kufanyia shughuli za biashara;

"takangumu" ina maana taka zote zinazozalishwa majumbani, kwenye taasisi, maeneo ya biashara na viwandani pamoja na takataka zote zilizofichana mahali popote zisizostahili, lakini haihusishi maji au taka miminika;

"taka za majumbani" maana yake ni taka za kawaida zilizozalishwa kwenye nyumba za kuishi;

"taka za biashara" maana yake ni taka zote zile zitokazo kwenye maeneo ya biashara au viwanda kwa kuzalishwa na viwanda vyenyewe au wakati huduma zinapotolewa ambazo sio kwenye makazi ya watu na hujumuisha taka nyingine zote ambazo sio za majumbani;

"taka hatari" maana yake ni taka zenye sumu, zinazoweza kuwaka moto, zinazoweza kula mwili au vyuma, zenye mionzi ya kurunuturisha (radioactive), zinazoweza kulipuka au taka zilizo hatari kama ilivyobainishwa na taasisi ya kulinda mazingira ya Tanzania (Tanzania Environment Protection Agency) inajumuisha mafuta ya dizeli, mafuta ya taa, petroli, rangi, mafuta ya kuyeyushia (solvent), betri za tochi, betri za magari, madawa ya kuulia wadudu waharibifu, na taka za hospitali au zinazoambukiza maradhi kutoka hospitali na zahanati, mafuta mazito ya kuteleza, pamoja na mafuta ya kulainisha na kuchanganya na vitu vingine kutoka kwenye viwanda, asbestos taka za kugeuza umbile, mizoga au maiti;

"upande wa mbele wa nyumba" maana yake ni eneo lote la mbele ya nyumba na eneo lililoko kati ya nyumba na barabara inayopakana na nyumba hiyo au kuungana na eneo la nyumba pamoja na eneo la hifadhi ya barabara linalopitisha maji ya mvua hadi katikati ya barabara hiyo;

"wakala" maana yake ni mtu yeyote, kikundi cha watu au kampuni iliyoteuliwa na Halmashauri kutoa huduma za usafi wa mazingira kwa niaba yake.

Uwezo wa Afisa Muidhiniwa

4. Afisa Muidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo lolote wakati wa saa za kazi kwa nia ya kukagua chukizo na kutoa taarifa ya maandishi kwa mmiliki wa eneo hilo kumtaka aondoe chukizo hilo.

Kutupa takataka

5. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka kutupa takataka, zitakazosababisha chukizo katika mitaa, uchochoro au eneo lolote lililokatazwa na Halmashauri.

Vyombo vya kuhifadhia takataka

6.-(1) Itakuwa niwajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba:-

(a) anaweka chombo cha kuhifadhia takataka chenye ukubwa unaotosheleza kila siku katika nyumba hiyo;

(b) takataka hizo zitatolewa nje pindi gari la kuzisomba linapopita au kupelekwa kwenye ghuba za taka zilizopo mitaani.

Ada ya uzoaji takataka

(2) Halmashauri au wakala atatoa huduma ya ukusanyaji wa taka ngumu zitakazolipwa kwenye majedwali ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Halmashauri itaweka mipango na utaratibu wa ukusanyaji na utupaji taka kutoka kwenye sehemu za biashara na nyumba za kuishi na kuzitoa taka hizo kuzitupa.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2), marufuku kwa mtu yeyote kuweka taka au maji machafu, kitu chochote au kemikali ambazo zinaweza kuleta madhara kwa binadamu au kusababisha moto katika chombo cha kuhifadhia takataka.

(5) Takataka zote zitatakiwa kuhifadhiwa ndani ya ua mpaka hapozitakapochukuliwa na Halmashauri au wenye nyumba au mpangaji kuzipeleka mwenyewe kwenye maeneo maalum yaliyotengwa.

Magari kuwa na vyombo vya kuhifadhia takataka

7-(1) Kila mmiliki wa basi litakaloingia katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwa na chombo cha kuhifadhi taka na kuhakikisha kwamba kila abiria anatupa taka kwenye chombo hicho.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mmiliki wa basi au dereva au kondakta iwapo abiria aliyepo ndani ya basi atatupa kitu chochote barabarani au stendi.

(3) Endapo abiria atakamatwa akitupa takataka nje ya basi la mmiliki wa basi au dereva au kondakta atawajibika kulipa faini ya papo kwa papo kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la IV la Sheria Ndogo hizi.

Uchomaji moto

8. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma takataka ovyo bila idhini ya Halmashauri.

Ukataji wa majani na kupunguza uzio

9. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba:-

(a) anakata majani yanayozidi kimo cha sm 5, aidha kukata uzio na kuondoa mabaki na kuyaweka kwenye chombo cha kuifadhia taka au sehemu iliyoruhusiwa kuhifadhi taka hizo;

(b) anafagia na kuondoa uchafu au malundo ya uchafu na kuweka safi eneo la mbele na nyuma ya nyumba yake;

(c) anatunza eneo lakichochoro linaloangukia upande wa nyumba yake.

Kutiririsha maji

10. Itakuwa ni marufuku mtu yeyote kumwaga, kutiririsha maji taka katika mtaa, uchochoro, eneo la wazi, mtaro ulio wazi au mashimo yasiyoruhusiwa.

Matumizi ya mashimo taka

11. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba kuunganisha mfumo wa maji taka kwenye mtaro wa maji taka endapo atashindwa kufanya hivyo atatakiwa kuelekeza uchafu katika mashimo ya maji taka yaliyoidhinishwa na Halmashauri.

Uchafuz wa maji

12. Itakuwa ni marufuku mtu yeyote:-

(a) kuchafua au kuvuruga maji yanayotumiwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu au wanyama;

(b) kuoga au kufulia kwenye chanzo cha maji, mto, bwawa au mfereji au tangi ambalo halikuwekwa kwa madhumuni hayo.

kuondoa chukizo

13. Endapo kutatokea chukizo lililosababishwa na maji taka katika nyumba yenye mpangaji zaidi ya mmoja na iwapo mwenye nyumba hawezi kupatikana kwa haraka, Halmashauri inaweza kuamuru wapangaji kufanya lolote linalowezekana ili kuondoa chukizo na gharama hizo zitahifadhiwa na mwenye nyumba.

Vyoo

14.-(1) Endapo Halmashauri itagundua kwamba nyumba inayokaliwa na mtu au watu haina choo au vyoo vyake viko katika hali ya uchafu au hatari kwa afya ya binadamu itatoa notisi ya siku 7 kwa wenye nyumba au mpangaji itamtaka kutengeneza vyoo hivyo kwa muda na kiwango kinachoridhisha kwa mujibu wa maelezo aliyopo katika notisi hiyo.

(2) Mtu yeyote anayemiliki jengo au nyumba inayotumika kama makazi atatakiwa kuweka vyoo vya kutosha na idadi ya watu wanaoishi katika nyumba hiyo kama atakavyoelekezwa na Halmashauri.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayemiliki kiwanda, shule, mgahawa, shule za bweni , hoteli au jengo lolote la umma, sehemu za burudani, au nyumba yoyote kuhakikisha kwamba vyoo vinavyoridhisha kwa ajili ya matumizi ya wanaume na wanawake na kwamba vyoo vina mwanga na hewa ya kutosha.

Uendeshaji wa Hoteli

(4) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya hosteli bila kibali cha Halmashauri.

(5) Kibali cha Hosteli ya wanafunzi au nyumba ya wageni

kitatolewa kwa kuzingatia yafuatayo:-

(a) mwanga na hewa ya kutosha;
(b) nafasi (space);
(c) vifaa (samani) vya kutosha;
(d) uimara wa jengo;
(e) uondoshaji wa maji taka, taka miminika na taka ngumu;
(f) usafi wa jumla wa majengo na vifaa vyake;
(g) utoshelezaji wa vyoo na bafu kwa jinsia zote.

(6) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayemiliki mgahawa wa vyakula au vinywaji kuhakikisha kuwa na vyoo vya kutosha kwa ajili ya wateja, watumishi na wapita njia na kuzingatia jinsia.

(7) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufunga milango ya vyoo kwa kufuli la aina yoyote ile.

Matumizi ya vyoo vichafu

15.-(1) Halmashauri inaweza kufunga choo chochote ambacho ni kichafu au kinahatarisha maisha ya binadamu au hakitaruhusiwa kutumika mpaka hapo Halmashauri itakaporidhika na matengenezo yaliyofanyika.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote ya kuhifadhi kinyesi au maji taka kuchimba au kujenga shimo kwaajili ya kuhifadhi kinyesi au maji taka bila idhini ya maandishi iliyotolewa na Halmashauri.

Kutupa kinyesi

16. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa kinyesi, mkojo, mate au matapishi katika uchochoro, mtaani au eneo lolote lisiloruhusiwa.

Maji taka ya viwandani

17.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha kiwanda chochote kinachotoa maji taka bila kuwa na mitambo ya kusafisha maji taka hayo ambayo imeidhinishwa na Halmashauri.

(2) Mtu yeyote anayemiliki jengo au nyumba inayotumika kama makazi atatakiwa kuweka vyoo vya kutosha kulingana na idadi ya

watu wanaoishi katika nyumba hiyo kama atakavyoelekezwa na Halmashauri.

(3) Maji taka kutoka viwandani yatatakiwa kupimwa kila baada ya miezi mitatu kabla na baada ya kuyasafisha ili kuangaliwa ubora wake na maabara ya Serikali au maabara yoyote iliyoruhusiwa na Serikali na majibu au matokeo ya uchunguzi huo kupelekwa kwa Halmashauri.

Usafi wa maeneo

18.-(1) (a) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi wa mtaa eneo lake analoishi kufanya usafi kila siku;

(b) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi wa mtaa kushiriki katika usafi wa jumla utakaofanyika kila jumatano ya mwanzo wa mwezi.

(2) Mkazi wa mtaa ambaye hatajitokeza kwenye shughuli za kujitolea kufanya usafi katika mtaa wake bila sababu za msingi atakuwa ametenda kosa.

Magari mabovu

19. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote:-

(a) kutelekeza magari mabovu kwenye njia ya mguu, mtaa au vichochoro au mitaa iliyo wazi na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo;

(b) kutengeneza gari au mtambo kwenye eneo ambalo sio mahususi kwa shughuli hiyo au eneo ambalo sio mahususi kwa shughuli hiyo au eneo lisiloruhusiwa na Halmashauri;

(c) kuosha magari au mitambo ya aina yoyote ile katika eneo lisiloruhusiwa na Halmashauri.

Uwezo wa Kamati za Maendeleo za Mitaa na Kata

20.-(1) Kamati za maendeleo za Kata na Mtaa zitakuwa na uwezo wa:-

(a) kusimamia usafi wa Mazingira kwenye maeneo yao;

(b) kumtoza faini isiyozidi shilingi elfu kumi mtu yeyote atakayechafua mazingira.

(2) Endapo mkosaji hatakuwa na fedha ya kulipa faini mara atakapokamatwa, Kamati itakuwa na uwezo wa kukamata mali ya mdaiwa yenye thamani sawa na kiasi cha faini anayodaiwa.

(3) Kama mkosaji hana fedha wala mali Kamati ya Maendeleo ya Kata au Mtaa itampa adhabu ya kufanya usafi kwenye Kata au Mtaa kadiri itakavyoona inafaa.

(4) Fedha zitakazopatikana kutokana na faini zitatumika kwenye shughuli za maendeleo za Kata au Mtaa husika na zitatakiwa stakabadhi ya Kata au Mtaa husika.

(5) Mtu yeyote atakayemzuia mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata au Mtaa kuelekeza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa anatenda kosa.

Ujenzi au ukarabati wa jengo

21.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu au kikundi cha watu kubomoa jengo lolote kwa njia yoyote ile bila kupata kibali cha Halmashauri.

(2) Kabla ya kubomoa mmiliki wa jengo atalipia gharama za kuondoa vifusi na mabaki ya jengo kwa gharama zitakazotathminiwa na Halmashauri.

(3) Mtu yeyote anayetaka kujenga au kukarabati jengo lolote atatakiwa kuhifadhi vifusi na vifaa vingine vya ujenzi ndani ya eneo au kiwanja chake na sio barabarani au kwenye ifadhi ya barabara.

Ufungaji wa mazao Ujenzi wa mazao

22.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa mzalishaji, mfanyabiashara au mchuuzi wa mazao au vitu vinavyoharibika kwa haraka kuingiza sokoni vitu hivyo vikiwa vimefungwa au kufunikwa kwa nyasi, majani ya mti au aina nyingine yoyote ya sehemu ya mmea.

(2) Afisa muidhiniwa atakuwa na uwezo wa kutekeleza aina ya chombo kitakachotumika kupakia mazao au vitu vinavyoweza

kuharibika endapo mazao hayo yatatakiwa kuletwa ndani ya eneo la Halmashauri na itakuwa ni wajibu wa kila mzalishaji, mfanyabiashara au mchuuzi kuhakikisha anafuata maelekezo hayo.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha (1) na (2) hapo juu, Halmashauri inaweza kusitisha uingizaji au kuamrisha kutolewa, aina yoyote ya mazao au vitu vinavyoharibika kutoka kwenye masoko.

Ufugaji mjini

23.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mfugaji wa wanyama kuhakikisha kwamba anakusanya na kuhifadhi uchafu wowote utokanao na wanyama hao kama vile kinyesi, manyoya, utumbo, baada ya kuchinjwa, na uchafu utokanao na ufugaji huo mfano nyasi au mabaki ya vyakula vyao katika hali ambayo haitaleta kero kwa jamii.

(2) Ufugaji unaoruhusiwa na Halmashauri ni ufugaji wa ndani (zero grazing) na sio kuzurura ovyo.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetaka kuendesha shughuli za ufugaji katika eneo la Halmashauri kuhakikisha kwamba ana eneo la kutosha.

(4) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufuga wanyama kwenye eneo la msongamano wa makazi (high density area).

Ukusanyaji wa madeni ya ada ya uzoaji taka

24.-(1) Halmashauri itakusanya madeni ya ada ya kuzoa taka kutoka kwa mmiliki kwa kumpelekea Hati ya Madai kwa maandishi na endapo atashindwa kulipa kwa muda wa siku 14 Halmashauri inaweza kufungua kesi ya madai Mahakamani au kukamata mali ya mdaiwa yenye thamani sawa na kiasi cha ada anachodaiwa.

(2) Mali iliyokamatwa itauzwa kwa mnada wa hadhara iwapo mhusika hataikomboa ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ilipokamatwa.

Uteuzi wa wakala

25.-(1) Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi kwa niaba yake.

(2) Wakala atakayeteuliwa atakuwa na wajibu wa:-

(a) kumchukilia mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha taarifa ya idadi ya watu waliopata ushuru na kiasi alichokusanya.

Viwanja visivyoendelezwa

26. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote anayemiliki kiwanja chochote au sehemu ya kiwanda ambacho hakijaendelezwa kutupa takataka kwenye viwanja au barabara zinazozunguka viwanja hivyo.

Wajibu wa kuwakilisha

27. Utakuwa ni wajibu wa kila mpangaji au mmiliki wa nyumba ya makazi au barabara kumwakilisha mmiliki au mpangaji wa nyumba chini ya Sheria Ndogo hizi kwa makosa atakayofanya mmiliki au mpangaji wa nyumba hiyo.

Jukumu la CBO's

28. Kutakuwepo na CBO's zitakazokuwa zinafanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa Maji katika Mitaa au Kata zao. CBO zitawajibika kukusanya taka ngumu na kuzipeleka kwenye jaa (dampo) pamoja na kukusanya ada za taka ngumu katika maeneo wanayotoa huduma.

Jukumu la Kamati za Maendeleo za Kata

29.-(1) Kamati za Maendeleo za Kata zikisaidiwa na Kamati za Mitaa zitakua na wajibu wa kusimamia shughuli zote za usafi pamoja na kulinda utekelezaji wa maslahi ya CBO's na Halmashauri.

(2) CBO's zitaingia mkataba na Halmashauri wa kuendesha aina ya shughuli ya usafi wa Mji au kudhibiti taka ngumu kama watakavyoelekezwa na Halmashauri.

Jukumu la Halmashauri

30. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kuhamasisha uundaji wa CBO's, kuzitambua, kuzipa nguvu za kisheria na kuziwezesha kuanza kazi.

Kufunga mgahawa au hoteli

31. Halmashauri inaweza kufunga mgahawa au hoteli yoyote ambayo mmiliki wake ameshindwa kuzingatia kanuni za afya mpaka hapo atakaporekebisha kasoro kama atakavyoelekezwa na Afisa Muidhiniwa.

32.-(1) Katika kuhakikisha kuwa shughuli za usafi zinafanyika kwa ufanisi, eneo la Halmashauri linagawanywa katika kanda na zitajulikana kama kanda A, B na C.

(2) (a) Wakazi wa kanda A watatakiwa kuchangia shs. 1,000/= kwa mwezi kama ada ya takataka;

(b) Wakazi wa kanda B watachangia shs. 500/=;

(c) Wazazi wa kanda C watachangia shs. 200/=.

Ulipaji wa ada kwa wafanya-biashara

33. Kila mfanyabiashara katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri atawajibika kulipa ada ya uzoaji taka kama inavyoonyesha kwenye jedwali la kwanza.

Ulipaji wa ada kwa makam-puni, viwa-nda na Taasisi zisizo za kiserikali

34. Kila mfanyabiashara katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri atawajibika kulipa ada ya uzoaji taka kama inavyooneshwa kwenye jedwali la pili na makampuni yoyote ambayo hayajaoneshwa yatakayoanzishwa.

Kadi ya ukaguzi wa afya

35.-(1) Kila nyumba yenye biashara au sehemu ya biashara itakuwa na kadi ya afya ya mwaka wa leseni unaohusika na kadi itawekwa wazi sehemu inayoonekana katika kipindi chote cha biashara.

(2) Bila kuathiri Sheria nyingine yoyote, hakuna biashara itakayoendeshwa bila kuwa na kadi ya afya iliyowekwa sehemu inayoonekana katika kipindi chote cha biashara.

(3) Halmashauri itatoza ada ya kadi ya afya kwa kila mwaka wa fedha kwa viwango vilivyooneshwa katika jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi.

(4) Mfanyabiashara atakayeshindwa kulipa na kupata Kadi kwa muda uliopagwa na Halmashauri, atatozwa adhabu ya 25% ya ada yake ya mwaka ambazo zitalipwa pamoja.

Makosa na adhabu

36. Mtu yeyote ambaye:-

Kufifilisha kosa

(a) atamzuia Afisa muidhiniwa kukagua nyumba, mgahawa, karakana, viwanda au nyumba ya biashara;

Uchangiaji wa huduma ya usafi

(b) atashindwa kuzingatia kanuni za afya na kusababisha magonjwa;

(c) atatupa au kuchoma taka ovyo;

(d) ataendesha kiwanda bila kuwa na mitambo ya kusafisha maji taka;

(e) ataweka magari mabovu kwenye maeneo yasiyoruhusiwa;

(f) atatupa taka kwenye kiwanja ambacho hakijaendelezwa, barabara au eneo la wazi;

(g) ataelekeza maji taka kwenye vyanzo vya maji;

(h) atafunga mitambo au vyombo vya usafiri vinavyochafua hewa kwa kutoa moshi mzito;

(i) atakiuka mojawapo ya Sheria Ndogo hizi;

(j) hatakuwa na choo katika maeneo ya makazi, taasisi maeneo ya biashara.

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo cha miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

37. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini ya papo kwa aina ya makosa ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira endapo mkosaji atakiri kutenda kosa hilo kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye Jedwali IV na kukubali kulipa kiasi cha faini anachodaiwa.

MGAWANYO WA MAENEO KIKANDA YATAKAYOHUSIKA NA UCHANGIAJI WA HUDUMA YA USAFI WA MJI

(Hii ni kwa wajibu wa Kifungu cha 32 cha Sheria Ndogo hizi)

38. Uchangiaji wa huduma ya usafi wa Mji umegawanywa kikanda ambapo kutakuwa na Kanda A, Kanda B na Kanda C.

(a) Kanda A itachangia Tsh. 1,000/=
(b) Kanda B itachangia Tsh. 500/=
(c) Kanda C itachangia Tsh. 200/=

Mgawanyo wa Kanda hizo ni kama ifuatavyo:-

KANDA A

KATA	KITONGOJI
1. Bariadi	1. Bariadi Kaskazini 2. Bariadi Mjini 3. Bariadi Kati 4. Viwandani 5. Salunda A 6. Salunda B 7. Kidinda 8. Mnadani 9. Buzunza

2. Sima	1. Salunda 2. Butiama 3. Budeka 4. Lyalu 5. Maelewano 6. Sima C 7. Sokoni
3. Malambo	1. Malambo 2. Sima A 3. Sima B 4. Benki 5. Bariadi Shule ya Msingi
4. Somanda	1. Somanda Kati 2. Majengo 3. Shuleni 4. Bomani

KANDA B

Maeneo ya Centre Zone	1. Nyangokolwa 2. Old Maswa 3. Nyakabindi 4. Mbiti 5. Guduwi 6. Bunamhala 7. Kilulu 8. Mahaha 9. Sanungu 10. Imalilo 11. Giriku 12. Kidalimanda 13. Mwakibuga

KANDA C

Maeneo yote yaliyobaki ambayo hayajaainishwa kwenye A na B

JEDWALI LA KWANZA

Na.	Aina ya Biashara	Ada kwa mwezi	Ada kwa mwaka
1.	Pombe za kienyeji	1,000/=	12,000/=
2.	Maduka ya rejareja	2,000/=	24,000/=
3.	Mama, baba lishe	1,000/=	12,000/=
4.	Ghala za mbao	5,000/=	60,000/=
5.	Restaurant (mgahawa)	5,000/=	60,000/=
6.	Maduka ya jumla	5,000/=	60,000/=
7.	Nyumba za kulala wageni	5,000/=	60,000/=
8.	Mashine za kusaga	4,000/=	48,000/=
9.	Viwanda vya mikate		
10.	Mashine za kuranda mbao	5,000/=	60,000/=
11.	Ofisi	2,000/=	24,000/=
12.	Baa zote za pombe za kigeni/Grocery	5,000/=	60,000/=
13.	Viwanda vya uselemala	2,000/=	24,000/=
14.	Saloon/vinyozi	2,000/=	24,000/=
15.	Gereji ya magari/pikpiki	5,000/=	60,000/=
16.	Kuchoma mahindi	500/=	6,000/=
17.	Wauza barafu	500/=	6,000/=
18.	Maduka ya nyama	3,000/=	36,000/=
19.	Workshop welding	5,000/=	60,000/=
20.	Watengenezaji wakubwa wa barafu	3,000/=	36,000/=
21.	Wauza mkaa jumla	3,000/=	36,000/=
22.	Wauza mkaa rejareja	1,000/=	12,000/=
23.	Filing station	5,000/=	60,000/=
24.	Zahanati binafsi	5,000/=	60,000/=
25.	Hospitali/vituo vya afya binafsi	10,000/=	120,000/=
26.	Biashara ndogo ndogo zisizotajwa	1,000/=	12,000/=
27.	Ghala	10,000/=	120,000/=

28.	Viwanda	20,000/=	240,000/=
29.	Shule/vyuo binafsi	5,000/=	60,000/=
30.	Mafundi cherehani	1,000/=	12,000/=
31.	Vizimba sokoni (kila kimoja)	100/=	1,200/=
32.	Depo (TBL, COCACOLA/ PEPSI, SERENGETI, MAJI)	10,000/=	120,000/=
33.	Kumbi za starehe		
34.	Na viwanda vingine vitakavyoanzishwa		
35.	Vibanda vya simu		
36.	Wauzaji wa ngozi		

JEDWALI LA PILI

Na.	Jina la Kampuni/ Viwanda	Ada kwa mwezi	Ada kwa mwaka
1.	TTCL	10,000/=	120,000/=
2.	BENKI	10,000/=	120,000/=
3.	POSTA	10,000/=	120,000/=
4.	TANESCO	10,000/=	120,000/=
5.	TANROAD	10,000/=	120,000/=
6.	MINARA YA SIMU	10,000/=	120,000/=
7.	Na mengine yatakayoanzishwa	10,000/=	120,000/=

JEDWALI LA TATU

Na.	Jina la Biashara	Ada ya kadi ya afya kwa mwaka
1.	Maduka ya jumla	6,000/=
2.	Nyumba za kulala wageni	6,000/=
3.	Mashine za kukoboa mpunga	50,000/=
4.	Pombe za kienyeji	2,000/=
5.	Maduka ya reja reja	3,000/=

6.	Mama/baba lishe	2,000/=
7.	Ghala za mbao	3,000/=
8.	Viwanda vya mikate	4,000/=
9.	Mashine za kuranda mbao	5,000/=
10.	Ofisi	3,000/=
11.	Baa zote za pombe za kigeni/ grocery	6,000/=
12.	Viwanda vya seremala	5,000/=
13.	Saloon/ vinyozi	5,000/=
14.	Gereji	10,000/=
15.	Maduka ya nyama	5,000/=
16.	Workshop/ Welding	4,000/=
17.	Watengenezaji wa barafu	4,000/=
18.	Wauza mkaa jumla	4,000/=
19.	Vituo vya kuuzia mafuta	15,000/=
20.	Zahanati binafsi/vituo vya afya	10,000/=
21.	Ghala	10,000/=
22.	Viwanda	50,000/=
23.	Shule/vyuo binafsi	10,000/=
24.	Mafundi cherehani	4,000/=
25.	Maduka ya dawa madogo	2,000/=
26.	Maduka ya madawa (pharmacy)	10,000/=
27.	Grocery bila vileo	5,000/=
28.	Wauza samaki/ dagaa	5,000/=
29.	Nyumba za video/sinema	5,000/=
30.	Mashine za kusaga	5,000/=
31.	Dry clinner	15,000/=
32.	Wakala mbali mbali	5,000/=
33.	Studio za picha	5,000/=
34.	Hoteli kubwa	10,000/=
35.	Maduka ya stationery	5,000/=
36.	Huduma za compyuta	2,000/=
37.	Migahawa	5,000/=
38.	Car wash	5,000/=
39.	Kumbi za starehe	10,000/=

JEDWALI LA IV

Hati ya Kukiri Kosa

(Chini ya kifungu cha 37)

Mimi .....nakiri mbele ya

.....(Mkurugenzi wa mji wa Bariadi kwamba mnamo tarehe.....

ya mwezi.....mwaka.....nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha.....

cha Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Mji wa Bariadi za mwaka 2012. Nipo tayari kulipa kiasi cha ushuru ninachodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 37 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kwa kadri ya ufahamu wangu

Tarehe.....saini.....

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo Tarehe 11, Desemba 2012 na Nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

.....
ERICA MUSSIKA,
Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji Bariadi

.....
ROBERT LWEYO MGATA,
Mwenyekiti
Halmashauri ya Mji Bariadi

Dar es Salaam,
15 Machi, 2013

MIZENGO PETER PINDA,
Waziri Mkuu